# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Julai 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580283

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Tundu Lissu afunguka kuhusu Membe

UKURASA 3



Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Matokeo jamii inapochoka watoto 'kusota' chini ya miti

Wanasayansi na tahadhari binadamu wanavyoangamiza

SAYANSI

NA MICHAEL ENEZA

Kitendawili cha COVID-19 virusi vinavyoibuka inapotimu miaka

UKURASA 11

# NEC yatangaza ajira 300,000 uchaguzi mkuu

**MAJIMBO** kubaki kama yalivyo, baadhi kubadilika majina, idadi ya vituo yawekwa wazi...*Endelea ukurasa 2*



Wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakipiga kura za maoni za wagombea wa ubunge wa Jimbo la Kinondoni, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## AHUKUMIWA KUNYONGWA KWA KUUA MKE, WATOTO

UKURASA 3

# Kutumia taarifa za NIDA sasa mpaka kulipia fedha

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** YANGA: SABABU KIPIGO SIMBA HII UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Ajira 390,000 zaja uchaguzi mkuu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), inatarajia kutangaza hivi karibuni mabadiliko ya majina kwa baadhi ya majimbo, huku akisema kuwa inatarajia kutoa ajira kwa watu 390,824 watakaoshiriki usimamizi wake kwenye vituo 75,000.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, aliyasema hayo jana alipohojiwa na Kituo cha Televisheni cha Clouds, akibainisha kuwa katika uchaguzi huo, hakutakuwa na punguzo au nyongeza ya majimbo.

Alisema majimbo yatabaki 364. Kati yake, ya Tanzania Bara ni 214 na Zanzibar ni 50 huku kata zikiwa ni 3,956.

"Tume mwaka huu haikuweza kuongeza majimbo, inabaki kuwa na majimbo 214 Bara na 50 Zanzibar na tunaenda kuyatangaza hivi karibuni majina ya majimbo hayo na kata 3,956 kutangazwa, hakuna mabadiliko, mabadiliko yatakayotokea ni majina tu," alisema.

Kuhusu maandalizi ya uchaguzi huo, mkurugenzi huyo alisema tume inatarajia kuwa na vituo 75,000 na kila kituo kinakuwa na watu watano.

"Hao watu watano ni msimamizi wa kituo cha kupigia kura, anasaidiwa na wasimamizi wawili, karani mwongozaji na mlinzi, hivyo kutakuwa na watumishi 390,824 kwenye vituo hivyo 75,000," alisema.

Alibainisha kuwa tume inatarajia kutoa tangazo la watu wenye sifa za kusaidia majukumu ya tume kwenye uchaguzi mwishoni mwa mwezi ujao.

"Watendaji wote wanaoteuliwa kushiriki masuala ya uchaguzi, tume ina bajeti ya kutoa elimu na kuwajengea uwezo wa kujaza fomu hizo vizuri na tangazo litatangazwa kwenye ngazi ya majimbo, na watakaowafanyia usahili ni ngazi za majimbo," alisema.

Kuhusu kuchelewa kwa ratiba ya uchaguzi, mkurugenzi huyo alisema tume inafanya majukumu yake kwa mujibu wa sheria na inasubiri tangazo kwenye gazeti la serikali la kuvunja Bunge ndiyo itoe ratiba hiyo.

"Tunasubiria wakati wowote tukishaliona tangazo, ndiyo tume inakuwa na uhuru wa kutoa tarehe ya uchaguzi, na kutangaza ratiba ya uchaguzi na kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, baada ya kutolewa tangazo la serikali si chini ya siku tano na si zaidi ya siku 25 NEC inabidi itangaze siku ya uteuzi wa wagombea," alisema na kuwaomba wananchi kuwa na subira hadi tangazo hilo litakapotolewa.

"Haiwezi kufika Desemba na kwa tamaduni za kitanzania, uteuzi umekuwa ukifanyika Agosti na uchaguzi Oktoba, hatujui tunasubiri hiyo siku tukijua tutaita vyombo vya habari kutangaza.

"Hakuna ucheleweshaji wa ratiba maana sheria imetubana, tunasubiri mamlaka ya kuvunja Bunge ionekane kwenye gazeti la serikali na itakapotoka, sheria inakubana kama imetoka leo tuhesabu siku tano na isizidi siku 25 uwe umefanya uteuzi."



Rais John Magufuli akiagana na Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, aliyeambatana na mkewe Regina, baada ya hafla ya chakula cha mchana aliyowaandalia wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), nyumbani kwake katika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma juzi. Kushoto ni mke wa Rais, Mama Janeth Magufuli. **PICHA: IKULU**

# Taarifa za NIDA sasa kwa malipo

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imesema kuanzia mwezi huu, itaanza kutoza fedha taasisi zote za umma na binafsi zinazotumia taarifa za mamlaka hiyo kuhudumia wananchi.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa NIDA, Geofrey Tengeneza, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, maarufu Sabasaba.

"Kuna wadau ambao wanatumia taarifa zetu kutoa huduma kwa wananchi, ninapenda niwajulishe kuwa kuanzia mwezi huu (Julai 2020), tunaanza kutoza tozo kwa taasisi zote za umma na binafsi ambazo zinatumia taarifa zetu kuhudumia wananchi.

"Kwa mfano, kampuni za simu, NSSF, Mfuko wa Bima ya Afya, benki na wadau wengine mbalimbali ambao ili watoe huduma kwa wateja wao wanahitaji kupata taarifa kutoka kwetu, ni lazima kuzilipia ili kuendelea kutoa huduma hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa taasisi hizo zinapaswa kuingia mkataba na NIDA ili kupata huduma hizo, vinginevyo taasisi ambazo zitashindwa kutimiza matakwa hayo, zitasitishiwa huduma hiyo mara moja.

Aliongeza kuwa tayari wametoa notisi kwa kampuni ambazo hazijaingia mkataba na NIDA kufanya hivyo mpaka Julai 31, mwaka huu, ili zikishindwa wasitishe huduma.

"Kampuni 17 tayari tumewatumia notisi kuanzia Agosti Mosi kama watakuwa hawajaleta maombi kwetu ili kuwapatia mkataba, tutawakatia huduma. Pia tunaendelea kufanya upembuzi kujua ni kampuni gani wanatumia huduma zetu," alisema.

Alisema kuwa kwa hatua ya awali wanategemea kuingia mkataba na watumia taarifa za NIDA ambao kampuni na taasisi 86.

Alisema kuwa utaratibu huo ni maelekezo kutoka kwa serikalini iliyoitaka NIDA kuanza kujitegemea kukusanya fedha kutumia utaratibu huo, ili kuondokana na utaratibu wa kupata fedha za matumizi kutoka serikalini.

"Mpaka sasa, kampuni 65 zimeleta maombi ya kutia saini mkataba na pia tumepeleka mikataba kwa kampuni 36 ambazo bado hawajarudisha. Pia kampuni 18 wamerudisha mikataba na 12 kati yao tayari tushasaini nao mkataba," alibainisha.

# Makatazo manne watiania CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), leo kinafungua dirisha la mchakato wa uchukuaji na urejeshaji fomu kwa watiania ya udiwani, ubunge na uwakilishi, huku kikitoa makatazo manne kwao.

Miongoni mwa makatazo hayo ni watia nia kutotumia mabango au vipeperushi hadi pale chama kitapopitisha mgombea wa eneo husika.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema CCM pia inazuia michango holela katika uchaguzi huo, huku akisema michango yote ni lazima ijadiliwe na ipitishwe na Kamati ya Halmashauri Kuu ya eneo husika.

"Licha ya kwamba kamati za siasa zina mamlaka ya kuweka mapendekezo ya michango, hii ninapenda ifahamike michango ya aina yoyote kwa wanachama inabaki wakati wote kuwa ya hiari, ni marufuku mwanaCCM kulazimishwa kutoa michango," alisema na kuonya mchango kuwa kigezo cha kumnyima mgombea fomu.

"Mtu akishachukua fomu, unaweza kusema chama kimepitisha harambee ya kuchangia, na iwe hiari yake kuchangia au kutochangia ndani ya vikao, tutajua huyu anajitoa kwenye chama au hajitoi," alisema.

Polepole alibainisha gharama za fomu ya udiwani kuwa ni Sh.10,000 na ubunge au uwakilishi ni Sh.100,000, huku akikumbusha katazo lingine kwa watia nia kujihusisha na vitendo vya rushwa.

"Makatazo yaliyopo ni pamoja na matumizi ya mabango au vipeperushi, kinaweza kuwa cha mtandao, nimeona kwenye mitandaoni watu wanatangaza nia, hilo ni kosa, ni kufanya kampeni kabla ya wakati huko ni kujipitisha kimtandao," alisema.

"Pia, wewe mwenyekiti ndiyo unasimamisha serikali, ukaamua kwenda kugombea. Ikiwa kugombea kwako kunazorotesha chama, hatutakuteua, we kachukue fomu," alisema.

Alisema katika mchakato huo, kutakuwa na uwazi na utafanyika hadharani kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa mgombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho.

"Mchakato wa kupiga kura za maoni uwekwe dhahiri shahiri hadharani, kuweka masanduku ya kura mbele ya wajumbe, na wale waliogombea washiriki kuhesabu. Tunataka mchakato uwe huru, wazi na haki," alisema.

Katika hatua nyingine, Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Elirehema Nassari, alisema jana kuwa wanachama 103 wametia nia kuwania ubunge katika majimbo 10 ya mkoa huo.

# Lissu atoa neno Membe upinzani

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amezungumzia uamuzi wa Benard Membe kujiunga na upinzani kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Membe, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika awamu iliyopita ya serikali, tayari ameshatangaza kujiunga na upinzani na mwishoni mwa wiki alikuwa na mazungumzo na uongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo ambako inadaiwa atawania kiti cha urais kupitia chama hicho.

Juzi, Nipashe ilizungumza na Lissu kwa mtandao akiwa nje ya nchi, akisema kutua kwa Membe upinzani kipindi hiki hakuwezi kuvuruga mipango ya vyama vya upinzani.

"Membe hawezi kuleta mgawanyiko wowote. Yeye ni mwanachama mpya wa ACT, siyo wa CHADEMA. Hawezi kuleta mgawanyiko kwetu (CHADEMA)," Lissu alisema.



Lissu anayesifika kutokana na utaalamu wake katika tasnia ya sheria, pia alizungumzia mchakato wa kumpata mgombea wa urais kupitia CHADEMA, akisema atampa ushirikiano mgombea atakayepitishwa ikiwa chama kitaona yeye hafai kupeperusha bendera yake.

"Kwanini (watia nia wengine) wanipe tabu kaka Enock (mwandishi)? Hatugombani, tunatafuta mwanachama anayeweza kustahimili mapambano makali yaliyoko mbele yetu.

"Inawezekana kabisa kaka Enock nisiwe mimi. Wapo watia nia 11 na mimi ni mmoja tu miongoni mwao," Rais huyo wa zamani wa Chama cha Wanasheria Tanganyika alisema.

Lissu, yuko nje ya nchi tangu usiku wa Septemba 7, 2017 aliposafirishwa kwa dharura kwenda jijini Nairobi, Kenya na baadaye Ubelgiji kupata matibabu ya kibingwa kutokana na kushambuliwa kwa kupigwa risasi nyumbani kwake Area D jijini Dodoma.

Hadi mwishoni mwa wiki, wanachama sita wa CHADEMA, akiwamo Lissu, walikuwa wamechukua fomu kuomba ridhaa ya chama hicho kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Mbali na Lissu, wengine ni Dk. Mayrose Majinge, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, Wakili Gaspar Mwalyela, aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita na Leonard Manyama.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kuua mke na watoto

**Na Neema Hussein, KATAVI**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Sumbawanga mkoani Rukwa, imemhukumu Yustine Robert (35) kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya kumuua mkewe na watoto.

Akisoma hukumu hiyo jana katika Mahakama ya Mhakimu Mkazi mkoani Katavi, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga, David Mrango, alisema mtuhumiwa alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 196 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Jaji Mrango alisema kwamba mtuhumiwa alitenda kosa hilo katika eneo la Majimoto Wilaya ya Mlele mkoani Katavi Aprili 5, 2013 kwa kuwatupa kwenye kisima cha maji mkewe na watoto wake wawili.

Ushahidi uliotolewa na mashahidi wa nne wa upande wa mashtaka ulionyesha kuwa mtuhumiwa alikuwa na ugomvi wa kifamilia siku moja kabla ya vifo vya wanafamilia wake.

Mrango alieleza kuwa mashahidi hao walisema kuwa mtuhumiwa alisikika akisema atafanya tendo la kihistoria ambalo halijawahi kutokea katika eneo hilo.

Jaji Mrango alisema ushahidi ambao umemtia hatiani Yustine Robert ni ushahidi wa kimazingira, ambao umetosha kuthibitisha shtaka aliloshtakiwa nalo mtuhumiwa.

Naye Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lugano Mwasubila, aliishukuru mahakama kwa kutenda haki ikiwa na kuitaka jamii kutokujichukulia sheria mkononi bali kuiacha sheria kuchukua mkondo wake.


UBALOZI WA NORWAY
NA
EUROPEAN UNION DELEGATION
DAR ES SALAAM

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Norway na European Union** watauza kwa mnada wa hadhara **Fanicha za nyumbani, ofisi na Magari tarehe 18 July,2020 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi.** Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.
Fanicha na Appliances zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Chest drawer, Coffee table, Dining table, Book shelve, Conference table, Office desk, Chairs, Vitanda, Magodoro, Zanzibar beds,Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, Gas & electric cooker, A/c split units, Photocopy m/c, TV set, Computer set, Voltage Stabulizer 30kva,Gym Cycle na vingine vingi.

**Magari yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado S/ Wagon | TA-VZJ120W | 2004 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Pathfinder Station Wagon | YD25 Diesel Engine | 2013 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Terrano Station Wagon | Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Mitsubishi Min Bus | 2.5 Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Mitsubishi Pickup Double Cabin | 4D56 Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Mercedes Benz Station Wagon | ML 270 Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Honda CR-V Station Wagon | K25A Petrol Engine | 2005 | Haujalipwa |
| 1 | Mobile Podium Trailer | 2Tons Trailer | - | Umelipwa |
| 3 | Generator 2.8, 2.4 & 1.7 KVA | Diesel & Petrol Engine | - | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 15 mpaka 17 July, 2020, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 24 July, 2020 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za bank ya CRDB** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

115808702

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926, 0759 284 926 E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**


# Athari 6 kiuchumi za corona kwa SADC hizi

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, amesema corona imeleta athari sita za kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Akifungua kikao cha siku tatu cha maofisa waandamizi wa hazina na Benki Kuu ndani ya Jumuiya hiyo, alisema athari hizo zimegusa sekta mbalimbali.

Alizitaja ni kushuka kwa mauzo nje, kudorora kwa sekta za huruma na kuongezeka kwa madeni ya serikali hizo.

Nyingine ni kupungua kwa shughuli za kiuchumi, kuongezeka idadi ya wakopaji wanaoshindwa kurejesha mikopo katika sekta za fedha na kupungua kwa mapato ya ndani ya serikali.

James ambaye ni Mwenyekiti wa Maofisa Waandamizi wa Hazina wa SADC, alisema corona imeleta changamoto mpya katika kupiga hatua za maendeleo ya uchumi hasa katika kufikia malengo ya viashiria vya uchumi mpana katika Jumuiya.

"Ili kukabiliana na athari hizo, kuna haja ya nchi wanachama kutumia mifumo ya kitaasisi katika kutafuta njia mbadala zenye ubunifu, ili kuharakisha hatua za kuimarisha uchumi wa ndani ya Jumuiya.

"Kikao hiki ni njia muafaka katika kujadili changamoto za kiuchumi na kutoa mapendekezo ya kitaalam yatakayowezesha mikutano ya kamati ya mawaziri wa fedha na uwekezaji na magavana wa benki kuu," alisema.

Pia alisema changamoto nyingine ni utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa makundi ya kijangili.

"Tatizo hili limesababisha baadhi ya nchi wanachama kuingia katika orodha ya nchi zilizo kwenye athari ya kuingia kwenye vikwazo vya kimataifa kwa kushindwa kutimiza vigezo na masharti ya Kikosi cha Masuala ya Fedha," alisema

Alisema hali hiyo inaweza kusababisha kudorora kwa jitihada za kuvutia uwekezaji na kuathiri malengo ya jumuiya.

"Ninaziomba nchi wanachama kuungana kwa pamoja na kufanya uchunguzi wa namna ambavyo tutaweza kuzuia na kuondokana na tatizo hili kwa kushauriana na kubadilisha uzoefu ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili," alisema.

Kadhalika, alisema pamoja na mafanikio ya kiuchumi ndani ya Jumuiya, baadhi ya nchi hivi karibuni zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya ukuaji mdogo wa uchumi, kuongezeka kwa nakisi ya bajeti, kupungua kwa mapato ya serikali na kuongezeka kwa madeni yanayotishia utekelezaji wa azma ya maendeleo katika jumuiya.

Kuhusu mkutano huo ambao utakuwa wa siku tatu kuanzia jana, alisema utakuwa na ajenda sita na kuzitaja baadhi kuwa ni kupitia taarifa ya maendeleo ya sekta ya fedha ya magavana wa benki kuu.

"Kupitia taarifa ya utekelezaji wa masuala ya udhibiti wa fedha haramu, kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mfuko wa Maandalizi ya Miradi ya Maendeleo wa SADC.

"Kupata taarifa ya hatua iliyofikiwa katika uanzishaji wa Mfuko Maalum wa Kugharamia Miradi ya Miundombinu ya Usafirishaji wa Nishati ya Umeme, inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB)."

Pia, alisema ajenda nyingine ni kupitia taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya mkutano uliopita wa Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji uliofanyika Windhoek, Namibia mwezi Julai mwaka jana.

Kadhalika, alisema watapokea na kujadili taarifa ya hatua iliyofikiwa ya namna ya uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Kikanda wa SADC.

James alimshukuru Rais John Magufuli ambaye ni Mwenyekiti wa SADC, kwa kusimamia kwa ufanisi shughuli za jumuiya ikiwamo suala la fedha na uwekezaji.

Pia, alizipongeza baadhi ya nchi wanachama kwa uamuzi wao wa kufungua na kuendelea na shughuli za kijamii na kiuchumi wakati wanaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya corona.

HABARI KITAIFA

# Katavi walia vituo kukosa petroli

**Na Neema Hussein, KATAVI**

WAENDESHA vyombo vya moto katika Manispaa ya Mpanda, Mkoa wa Katavi, wameiomba serikali kuingilia kati suala la uuzaji wa mafuta ya petroli kutokana na vituo vingi vya uuzaji wa mafuta hayo kugoma kutoa huduma hiyo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, madereva hao walisema wanapoteza muda mwingi kupanga foleni kusubiri mafuta yanayotolewa na kituo kimoja katika manispaa hiyo. Doto Julius, dereva wa gari ya kutoka Mpanda kwenda Kasekese, alisema wakienda kununua mafuta kwenye baadhi ya vituo wanaambiwa hawauzi.

"Tunapata shida sana tunaenda kununua mafuta tunaambiwa hawauzi sijui ni kwasababu ya bei hadi ipande hatujui wengine wana mafuta, lakini hawataki kuuza," alilalamika Julius.

Meneja wa Kituo cha Mafuta Sereniva, Thomas Magabe, alisema kituo hicho kwa sasa kimekuwa mkombozi kwa madereva kutokana na vituo vingi kutouza.

Kwa upande wake ofisa huduma kwa wateja na utawala mkoa wa Rukwa, Ramadhan Kakende, alisema taarifa za kukosekana mafuta ndio anazisikia kwa mara ya kwanza na kuahidi kufanya mawasiliano na viongozi wa juu.

Hata hivyo alisema tatizo kama hilo lilitokea baada ya wiki mbili katika Mkoa wa Rukwa na baada ya kufanya utafiti walitambua kuwa wamiliki wa vituo hivyo wanakwamishwa na vituo vikubwa vya mafuta vilivyopo jijini Dar es Salaam, wakituma magari yao wanakataa kuwawekea mafuta.



Msururu wa waendesha bodaboda wakisubiri kununua mafuta ya petroli yanayouzwa kwenye kituo kimoja tu katika Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi jana, baada ya vituo vingine kugoma kutoa huduma hiyo. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

# Katibu Mkuu ACT ajitosa ubunge

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

WANACHAMA wawili wa chama cha ACT-Wazalendo, akiwamo Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, wamechukua fomu za kuomba kuteuliwa kupeperusha bendera ya chama katika kinyang'anyiro cha ubunge Tunduru Kaskazini.

Katibu wa ACT-Wazalendo Wilaya ya Tunduru, Fransis Kuvile, alisema jana kuwa mbali na Shaibu, Mwenyejiti wa Jimbo hilo wa ACT-Wazalendo, Usain Mawila, pia amechukua fomu.

Alisema watia nia hao walichukua fomu hizo juzi, akisema nafasi zipo wazi kwa wanachama wanaohitaji kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kupitia chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema tayari chama kimesambaza fomu za watia nia wa nafasi za udiwani katika kata zote 39 za majimbo ya uchaguzi ya Tunduru ambayo ni Tunduru Kusini lenye kata 15 na Tunduru Kaskazini lenye kata 24 .Alisema kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu, ACT-Wazalendo imejipanga kusimamisha wagombea katika majimbo yote na kata zake zote.

Katibu Bunge la 11 lililofungwa Juni 16 mwaka huu, ACT-Wazalendo ilikuwa na mbunge mmoja, Zitto Kabwe, aliyekuwa anawakilisha Jimbo la Kigoma Mjini.

**Kiongozi huyo alisema tayari chama kimesambaza fomu za watia nia wa nafasi za udiwani katika kata zote 39 za majimbo ya uchaguzi ya Tunduru ambayo ni Tunduru Kusini lenye kata 15 na Tunduru Kaskazini lenye kata 24 .Alisema kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu, ACT-Wazalendo imejipanga kusimamisha wagombea katika majimbo yote na kata zake zote.**

# Askofu Mdegella ataja sifa za uongozi wa kuchaguliwa

**Na Francis Godwin, IRINGA**

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, Dk. Owdenburg Mdegella, amesema jamii inahitaji kuwa na viongozi wabeba maoni yao na si wanaotafuta kuitumia jamii kupata mali.

Akizungumza jana wakati wa kipindi chake kinachorushwa na Radio Furaha na kituo cha matukio Daima Tv, Dk. Mdegella alisema kuwa suala la uongozi linahitaji mtu mwenye utayari wa kweli wenye uchaji wa kimungu katika kuwatumikia wananchi.

Dk. Mdegella ambaye ni mtiania wa ubunge Jimbo la Kilolo mkoani Iringa, alisema kuwa kwa upande wake haingii kuomba nafasi ya ubunge ili kwenda kujinufaisha bali anakwenda kuitumikia jamii.

Alisema kuwa upande wake amejitosheleza kwa mali mbalimbali anazomiliki yakiwamo mashamba, nyumba na magari na kuwa haendi katika ubunge kwa ajili ya kutafuta mali bali anakwenda kiwito kwenda kuwatumikia wananchi ili nao wafurahie matunda ya nchi yao na jitihada za serikali ya CCM chini ya Rais John Magufuli.

Alisema katika hali ya kawaida, uongozi wa kisiasa mtu yeyote anaweza kubahatisha, lakini sio uongozi wa kumtumikia Mungu ingawa asema wote wasaka uongozi ni vema wakajiuliza mbele za Mungu juu ya nafasi wanazoomba iwapo wanaweza kuzitumikia.

Dk. Mdegella alisema kila mmoja anamapungufu yake ya kibinadamu, lakini hakuna sababu ya kukata tamaa kutokana na mapungufu hayo badala yake kusonga mbele na kumtanguliza Mungu kwa kila hatua.

## Wahandisi wa ndani waifagilia serikali kuwajali

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imepongezwa kwa kuwapa nafasi wahandisi wa ndani ili kutekeleza baadhi ya miradi mikubwa ya kimkakati.

Mhandisi mshauri wa umeme ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya GEARED Consulting Engineers LTD, Mhandisi Warda Meshamark, ndiye aliyetoa pongezi hizo.

Amesema katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya tano imetambua uwezo mkubwa walionao wahandisi wa ndani na kutoa fursa ya kuwapa miradi mbalimbali mikubwa kuitekeleza.

Mhandisi Warda aliyasema hayo jijini Dar es Salaam kwa wanahabari ambapo alisema anaipongeza sana serikali kwa kuwaamini, huku akitolea mfano kampuni yake kupewa mradi mkubwa wa Hospitali ya Kwanga iliyopo Musoma mkoani Mara.

"Wazawa tunapewa fursa tena kubwa katika kipindi hiki hakuna longolongo kwani ukiwa na vigezo vyao tu unapata kazi bila shaka yeyote, mfano mimi licha ya miradi mingine mingi, lakini serikali imeniamini na hivi sasa kupitia kampuni yangu tunasimamia mradi mkubwa wa ujenzi wa Hospitali ya Kwanga iliyopo Msoma mkoani mara.

Aliongeza: "Najitahidi kukimbiza mradi ule ili uweze kukamilika mapema na wananchi wa Mkoa wa Mara na viunga vyake waweze kupata huduma pale kama serikali ilivyokusudia."

Pia alisema licha ya kusimamia miradi mbalimbali nchini, pia kampuni yake imeweza kuaminika na kupata kazi katika nchi jirani Malawi, Zambia na kungineko na hata visiwani Zanzibar.

# Ubunge CUF hadharani Julai 17

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema kinatarajia kuhitimisha kazi ya kura ya maoni kwa nafasi ya wagombea ubunge, Julai 17.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai, alisema wameshaanza mchakato huo.

"Tumeshaanza mchakato wa kura ya maoni kwa wagombea wa nafasi za ubunge na kwa baadhi ya mikoa tumeshamaliza, ni maeneo machache tu ambayo yamebaki ambayo mpaka kufikia Julai 17 tutakuwa tumemaliza, "alisema Kilaghai.

Pia, alisema kwa upande wa madiwani wameshamaliza kazi hiyo ya kura za maoni.

"Kwa madiwani tayari tumemaliza, tuna uhakika tutasimamisha madiwani zaidi ya asilimia 80 nchi nzima," alisema Kilaghai.

# Wanawake TADEA kumnadi JPM urais

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHAMA cha Tanzania Democratic Alliance (TADEA), kimeomba kushirikiana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika kampeni za kumnadi Rais John Magufuli kwenye uchaguzi mkuu, mwaka huu.

Ombi hilo lilitolewa jana na Katibu wa Wanawake wa chama hicho, Nuru Kimwaga, katika hafla ya kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, iliyoandaliwa na wanawake viongozi wa vyama vya siasa.

"Hii ndio Tanzania tunayoitaka na ili tuweke historia katika nchi yetu sisi kama wanawake au vyama vingine vya siasa katika uchaguzi wa 2020, tunaomba salamu hizi mfikishie Rais Magufuli kwamba tunataka kutengeneza historia vyama vya upinzani viweze kushiriki ya kumnadi," alisema.

Alisema wapo tayari kwenda mkoa hadi mkoa kuonyesha taswira ya Tanzania.

"Tunataka kuonyesha tunapeleka vipi Tanzania katika taswira ambayo bila kuiga utamaduni wa nchi nyingine kwa upendo na amani, watambue kwamba kuna chama cha siasa kipo tayari kushirikiana na CCM kufanya kampeni kutokana na yale mema yaliyofanywa na Rais," alisema.

Alisema maendeleo yaliyopatikana sio ya itikadi ya chama kimoja ni ya wote.

"Vyama hivi ni rafiki tunataka kwenda kirafiki kama ambavyo tulivyojengewa misingi hii na waliotutangulia," alisema. Akitoa ufafanuzi kuhusu vyama vinavyotaka kushiriki kampeni hizo, mratibu wa hafla hiyo, Saumu Radhid, alisema si vyama vyote isipokuwa ni vile vinavyotamani.

"Sisi tunachotaka ni ustaarabu kwenye kampeni zote, tunataka kampeni za kistaarabu, kuna baadhi ya vyama vinatumia wanawake kudai vitu fulani hili halikubaliki, tunaomba msajili wa vyama aliangalie hili wanawake wasitumike kuvuruga amani ya nchi yetu," alisema.

the Jane Goodall Institute Tanzania
*For Wildlife Research, Education & Conservation*

MIAKA 60 YA UTAFITI WA SOKWE MTU WA GOMBE

the Jane Goodall Institute GOMBE 60

Mnamo Julai 14, 1960 Jane Goodall akiwa na umri wa miaka 26 aliwasili katika pori la akiba la Gombe kuanza utafiti wa sokwemtu, utafiti ambao leo hii July 14 unatimiza miaka 60. Utafiti huu wa kipekee ni moja ya tafiti za muda mrefu za sokwemtu kuwahi kufanyika ulimwenguni.

Bodi ya wakurugenzi na wafanyakazi wa Taasisi ya Jane Goodall Tanzania, inapenda kutoa shukurani zake za dhati kwa serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Taasisi zote za serikali, zikiwemo Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori (TAWIRI), Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknologia (COSTECH) na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), wafadhili wa ndani na nje ya nchi, wadau na jamii zote zinazoizunguka hifadhi ya taifa ya Gombe kwa mchango mkubwa uliowezesha utafiti wa sokwemtu kutimiza miaka 60.

Utafiti wa sokwemtu unaoendelea bila kusimama kwa kipindi chote hiki umeuwezesha ulimwengu kuwafahamu vyema sokwemtu na uhusiano wao wa karibu na binadamu. Kati ya mambo muhimu yaliyoibuliwa katika utafiti huu ni pamoja na uwezo wa wanyama hawa kutengeneza na kutumia zana mbalimbali ili kukidhi maisha yao. Moja ya matokeo ya utafiti wa Jane Goodall ni ugunduzi kuwa sokwemtu wanaweza kuandaa kijiti na kukitumia kama zana ya kuvulia mchwa toka kwenye vichuguu na kutumia kama kitoweo. Uvumbuzi wa sokwemtu wanavyoweza kutengeneza na kuzitumia zana mbalimbali ulibadilisha mtazamo uliyokuwepo kwamba ni binadamu pekee aliye na uwezo wa kutengeneza na kutumia zana kutatua changamoto za maisha yake.

Tafiti hizi pia zimesaidia kuwafahamu zaidi viumbe hawa hususani maisha yao kitabia na mahusiano yaliyopo ndani ya kundi na baina ya makundi kama vile makuzi ya watoto, nafasi ya majike katika kundi na wanavyo shirikiana ndani ya kundi lao, lakini pia katika kupambana na makundi mengine ya sokwemtu ili kulinda maslahi ya makundi ya familia zao. Kwa kiasi kikubwa tabia hizi zimeonekana kufanana sana na zile za binadamu, ufahamu ambao huwezesha binadamu kujitambua zaidi kwa kupitia utafiti huu.

Pamoja na faida hizi za kisayansi, utafiti wa sokwemtu umetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa na jamii kwa ujumla; Kitaifa, filamu, vitabu na majarida mbalimbali kuhusu tafiti za sokwemtu wa Gombe vilivyo chapishwa na viliwafanya sokwemtu na Hifadhi ya Taifa ya Gombe kujulikana duniani kote. Filamu na machapisho haya yamekuwa kichocheo cha ukuaji wa utalii nchini hususani katika Hifadhi ya Taifa ya Gombe. Kwa muda wote huu, utafiti wa sokwemtu umekua ukifanyika kwa kuwatumia wazawa kutoka maeneo ya vijiji jirani ya hifadhi ya Gombe na hivyo kwa namna nyingine kuchangia maendeleo ya vijiji husika.

Kama ilivyo kwa jamii ya sokwemtu wengine katika bara la Afrika, sokwemtu wa Gombe wamekuwa wakipungua kwa kasi kutokana na uharibifu wa misitu waishimo na hivyo kuleta changamoto kuhusu mustakabali wa maisha yao. Kwa kutambua hili, Taasisi ya Jane Goodall kwa kupitia utafiti huu, ilianzisha mradi wa elimu ya mazingira kwa vijana mashuleni ujulikanao kama "Roots & Shoots" pamoja na mradi jumuishi wa hifadhi ya mazingira "Tanganyika Catchment Reforestation and Education" "TACARE". Miradi hii kwa pamoja imekuwa chachu ya hamasa kwa jamii katika kuzishughulikia changamoto za uhifadhi zinazowakabili sokwemtu, jamii zilizopo karibu na makazi ya sokwe na mazingira yao kwa ujumla. Roots & Shoots ina himiza vijana walio shule kutunza mazingira wakati TACARE inashirikiana na vijiji katika kutunza mazingira na kuanzisha miradi ya kuwaongezea kipato na hivyo kupunguza utegemezi wa maliasili kwa kiwango kikubwa. Shughuli hizi zimeanza kuzaa matunda.

Kwa kutambua umuhimu wa sokwemtu na changamoto zinazomkabili, mamalaka za uhifadhi za kimataifa zilipitisha azimio la kuifanya tarehe 14 Julai ya kila mwaka kuwa siku ya sokwemtu duniani. Siku hii iliadhimishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2018, lengo kuu likiwa kuchochea na kuhamasisha uelewa wa wananchi na jumuiya za kimataifa kuhusu umuhimu wa kuwahifadhi sokwemtu duniani. Kwa asili sokwemtu hupatikana katika bara la Afrika pekee.

Tunapoadhimisha miaka 60 ya utafiti wa sokwemtu, tunaamini bado kuna mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa wanyama hawa adimu ulimwenguni ambao kwa vinasaba wanafanana na binadamu kwa zaidi ya asilimia 98. Ukuaji wa tekinolojia umetuwezesha kujiuliza maswali kuhusu tabia na mwenendo wa sokwemtu ambayo mwanzoni yalikua magumu kuyajibu. Tekinolojia inatusaidia kujua zaidi mahusiano ya sokwemtu kwenye kundi lake, kwa mfano, jamii ya sokwemtu kwa kuangalia wanavyoishi pamoja na kuutambua mlolongo wa vinasaba katika jamii zao.

Hivyo basi ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunaendelea kuhifadhi misitu ili kuyalinda makazi yao ya asili na zaidi kumlinda sokwemtu ambaye yuko katika hatari ya kutoweka nchini kwetu. Kila mmoja wetu analo jukumu la kuwalinda sokwemtu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

P. O. Box 70728, Dar es Salaam, Tanzania, Tel: +255 22 277 5236; Fax: 255 22 277 5230
E-mail: jgi-tanzania@janegoodall.or.tz Website: www.janegoodall.org

215809902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua hii itaisaidia NIDA kutoa huduma kwa ufanisi

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imesema kuanzia mwezi huu, itaanza kutoza fedha taasisi zote za umma na binafsi zinazotumia taarifa za mamlaka hiyo kuhudumia wananchi.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa NIDA, Geofrey Tengeneza, aliyasema hayo juzi alipozungumza na wanahabari katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba).

Alisema kuna wadau ambao wanatumia taarifa za NIDA kutoa huduma kwa wananchi, na kuwa kuanzia mwezi huu, mamlaka hiyo itaanza kutoza tozo kwa taasisi zote za umma na binafsi ambazo zinatumia taarifa zake kuhudumia wananchi.

Miongoni mwa taasisi na kampuni ambazo zitatakiwa kutozwa ni kampuni za simu, NSSF, Mfuko wa Bima ya Afya, benki na wadau mbalimbali ambao ili watoe huduma kwa wateja wao, wanahitaji kupata taarifa kutoka NIDA, hivyo ni lazima kuzilipia ili kuendelea kutoa huduma hiyo.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, taasisi hizo zinapaswa kuingia mkataba na NIDA ili kupata huduma hizo, vinginevyo taasisi ambazo zitashindwa kutimiza matakwa hayo, zitasitishiwa huduma hiyo mara moja.

Imeeleza kuwa imeshatoa notisi kwa kampuni ambazo hazijaingia mkataba kutokana na NIDA kufanya hivyo hadi Julai 31, mwaka huu, ili zikishindwa zisitishiwe huduma.

Kimsingi, hatua hiyo itaisaidia mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yake kwa tija na ufanisi, kwa kuzingatia kuwa huko nyuma ilikuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa kiasi cha kusababisha isuasue katika utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi.

Changamoto kubwa ambayo imekuwa ikionekana kwa kila mmoja ni ufinyu wa bajeti kutokana na NIDA kutozalisha badala yake kutegemea fedha za ruzuku kutoka serikalini.

Matokeo yake ni kuwa mamilioni ya Watanzania waliomba vitambulisho muda mrefu, lakini hadi sasa hawajavipata, huku wakipewa ahadi zisizo na utekelezaji.

Hata ofisa huyo wa NIDA amefafanua kuhusiana na hilo kwa kusema kuwa utaratibu huo ni maelekezo kutoka kwa serikalini iliyoitaka mamlaka hiyo kuanza kujitegemea kukusanya fedha kutumia utaratibu huo, ili kuondokana na utaratibu wa kupata fedha za matumizi kutoka serikalini.

Tunaona kuwa uamuzi huo wa serikali ni mzuri, ingawa umechelewa kutolewa. Tunasema hivyo kwa kuwa kama ungetolewa mapema leo hii NIDA ingekuwa inajitosheleza kwa bajeti, hivyo kutekeleza majukumu yake kwa tija na ufanisi.

Kama mamlaka hiyo ingeelekezwa kujitegemea tangu kuanzishwa, ingekuwa na mapato yake kama zilivyo mamlaka nyingine nchini badala ya kutegemea kila kitu kutoka serikalini, zikiwamo fedha za mishahara, ununuzi wa vifaa na matengenezo yake. Kwa mfano, kwa muda mrefu NIDA imekuwa ikilalamikiwa na wananchi kukamilisha taratibu zote za kujiandikisha kwa muda mrefu, lakini hawapatiwi vitambulisho kwa maelezo kuwa mashine zimeharibika hadi hapo zitakapotengenezwa au kununuliwa mpya.


Usumbufu huo umekuwa ukiwafanya baadhi ya watu kukosa imani kwa mamlaka hiyo, huku wengine wakiiona kama haibadiliki badala yake kufanya kazi kwa mazoea.

Huduma ambazo zinatolewa na mamlaka hiyo kwa kampuni na taasisi za umma ni nyingi, hivyo kuna uhakika kwamba itakusanya mapato yatakayoiwezesha kujiendesha na kiasi kingine cha fedha kupelekwa serikalini.

Ushauri wetu kwa NIDA ni kuwa ikubali mabadiliko hayo kwa mtazamo chanya pamoja na kuwaandaa watumishi wake kuacha mtindo wa kufanya kazi kwa mazoea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




### Muungwana Lazima Nilonge



## Wazazi, walezi ufumbuzi taulo za kike usisahaulike

**Na Sabato Kasika**

UKOSEFU wa taulo za kike kwa baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini ni tatizo, ambalo linabuniwa kampeni mbalimbali kwa lengo la kulimaliza ili waweze kuhudhuria masomo bila kikwazo.

Miongoni mwa kampeni hizo ni ile ya 'mpe mabawa' ambayo imewahi kubuniwa na wadau wa maendeleo ya elimu kwa mtoto wa kike, ili asikae nyumbani kwa sababu ya hedhi.

Kampeni hizi ni wazi kwamba zinaweza kumweka mtoto wa kike katika mazingira salama yatakayofanya asome kwa kuhudhuria vipindi vyote awapo shuleni bila kikwazo.

Suala la uwazi ndilo lililopewa uzito kwenye kampeni hiyo kwa ajili ya kuondoa ukimya ili kuliongelea bila kificho, kuboresha mazingira ya shule kwa kuhakikisha upatikanaji wa vyoo ya kutosha, maji ya uhakika, taulo na sehemu za kujihifadhi na kujisitiri.

Kwa hali kama hii kama itazingatiwa, ni wazi wanafunzi wote wa kike wanaweza kuondokana na tatizo la kutohudhuria vipindi na kulazimika kukaa nyumbani.

Pamoja na hayo, ni jukumu la wazazi na walezi sasa kuwafundisha watoto wa kike kuhusu hali hiyo ili wanapokutana nayo wawe wazi kuwaeleza na kutafuta mbinu za kuwasaidia kuliko kukaa kimya. Kuna haja kwa wazazi na walezi kuweka mazingira ya kuwawezesha watoto wao kujitambua wanapofikia hatua hiyo.

Ninasema hivyo kwa sababu, uhaba na ukosefu wa taulo za kike umekuwa ukitajwa kukwamisha baadhi ya wanafunzi kuhudhuria vipindi shuleni. Hali kama hiyo ni hatari kwa maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike, hivyo kuna haja wadau wote wa elimu kuanzia kwa wazazi na walezi, kushiriki kikamilifu katika kumaliza tatizo hili.

Bila kufanya hivyo, watoto wa kike wanaweza kuendelea kubaki nyuma kielimu, kwa sababu ambazo wakati mwingine ziko ndani ya uwezo wa wazazi, walezi na jamii.

Kimsingi ni kwamba kampeni za kuhamasisha uchangiaji wa taulo za kike hufanyika mara kwa mara, lakini tatizo bado lipo, umefika wakati sasa wa kupatia tatizo hilo ufumbuzi wa kudumu.

> **Kimsingi ni kwamba kampeni za kuhamasisha uchangiaji wa taulo za kike hufanyika mara kwa mara, lakini tatizo bado lipo, umefika wakati sasa wa kupatia tatizo hilo ufumbuzi wa kudumu.**

Ufumbuzi huo unategemea wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kutambua kwamba ukosefu wa taulo za kike ni tatizo kwa wanafunzi kwa kusababisha wakose vipindi kila mwezi.

Hivyo kila mmoja aangalie uwezekano wa kumsaidia mtoto wake na kama hana uwezo wa kifedha, basi awe wazi ili zifanyike njia za kumwezesha kupata taulo hizo kwa ajili ya mabinti zake. Wazazi na walezi watimize wajibu wao wa kuhakikisha watoto wao wanasoma, ikiwamo ni pamoja na kuhakikisha wanapata taulo za kike za kuwawezesha kujihifadhi.

Iwapo kila mmoja atatimiza wajibu, mtoto wa kike atapunguziwa matatizo ambayo yamekuwa yakimkabili yakiwamo ya kukeketwa, kuolewa na kusababisha akatishe masomo.

Ufike wakati kila mmoja aseme sasa inatosha mtoto wa kike kukosa vipindi anapokuwa kwenye hedhi au kukatishwa masomo kwa sababu ya kukeketwa ama kuozwa, kwani wote wana haki ya kupata elimu kama walivyo wa kiume.

Watoto wote wana haki ya kupata elimu bila ubaguzi, hivyo jitihada ziendelee kufanyika ili kuwaondoa watoto wa kike kwenye tatizo la kukosa baadhi ya vipindi shuleni, kwa sababu ya hedhi.

Kwa wazazi wenye hali nzuri kiuchumi, wanaweza kuamua kununua taulo za kike kila mwisho wa mwezi na kuzipeleka, katika shule kwa ajili ya kuwasaidia mabinti ambao hawana uwezo wa kifedha.

Aidha, jamii itambue umuhimu wa kutoa fursa sawa kati ya mtoto wa kike na wa kiume, kupewa mafunzo ya stadi za maisha, kumtimizia mahitaji yote ya msingi kwa kuondoa unyanyapaa.

# DC aagizwa kukomesha mauaji Nzega

Na Tiganya Vincent, TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Advera Bulimba, kuhakikisha anakomesha vitendo vya mauaji vinavyotokana na wananchi kujichukulia sheria mikononi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kumwapisha Mkuu huyo mpya wa Wilaya ya Nzega anayekwenda kushika nafasi ya Godfley Ngupula.

Alisema wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo la baadhi ya watu kuamua kuwaua wenzao kwa imani za kishirikina na wivu wa kimapenzi, jambo linalotia doa mkoa.

"Nenda ukatumie uzoefu wako na mafunzo na ujuzi ulionao ukakomesha tabia ya baadhi ya watu kuamua kukatisha maisha ya wenzao...mkashirikiane na viongozi wenzao kuhakikisha tatizo hilo linakwisha na wananchi wote wanaishi kwa amani," alisema.

Alisema ni vema wakahakikisha wanasimamia haki na kufanyakazi kwa usawa ili wanyonge wanoanyanyaswa wapate kilimbilio na kupata majawabu ya kero zao ili wilaya hiyo iwe mfano kwa Mkoa wa Tabora.

Dk. Sengati alimtaka kuhakikisha anasimamia watumishi waliochini yake katika kujenga uchumi wa Wilaya ya Nzega na kuimarisha upatikanaji huduma bora kwa wananchi hasa kwa wale wanaoishi pembezeni.

"Nenda ukachape kazi ili uweze kuacha alama kama kielelezo cha utendaji wake kwa wananchi," alisema.

Aliwataka vijana walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali kuhakikisha wanafanyakazi kwa uzalendo na uadilifu ili kumwonyesha Rais John Magufuli kuwa hakukosea kuwaamini.

Naye Bulimba alimshukuru Rais Magufuli kwa kumwamini na kuweza kumteua kushika nafasi hiyo ya uongozi.

Aliahidi kuchapa kazi ya kuwatumikia wananchi kwa haki na usawa bila ya upendeleo ili kumwakilisha Rais ipasavyo katika wilaya hiyo.

Bulimba aliwataka kushirikiana naye katika kuhakikisha wanatatua matatizo ya wananchi ili waweze kufikia malengo yao.

Mkuu huyo wa Wilaya ya Nzega aliteuliwa hivi karibuni kuchukua nafasi ya mtangulizi wake Godfrey Ngupula ambaye amestaafu.

# Wabaini ubadhirifu TALGWU

Na Mary Geofrey

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), kimesema katika kipindi cha miaka minne ya uongozi uliopo madarakani, kimefanikiwa kubaini ubadhirifu wa fedha za chama uliofanywa na uongozi wa Taasisi ya Fedha ya TALGWU.

Imeelezwa kuwa, baada ya uchunguzi wa ubadhirifu kufanyika, uongozi wa juu ya Taasisi ya Fedha ya TALGWU ulisimamishwa kazi na baadaye kufukuzwa kabisa.

Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi na kusema kuwa pamoja na watumishi hao kufukuzwa kazi, vyombo vya dola vinaendelea na uchunguzi wa kina.

"Mnamo Oktoba mwaka 2018, uongozi wa chama uligundua kuna changamoto kwa upande wa uendeshaji wa taasisi na tulitoa maelekezo kwa Bodi ya TALGWU Microfinance kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kufanyika kwa ukaguzi maalum uliopelekea watendaji wakuu wa taasisi kusimamishwa kazi na hatimaye kuachishwa kazi," alisema.

Aliendelea kueleza kuwa tangu mwaka 2016, walifanikiwa kusimamia kesi 130. Kati yake, kesi zilizoisha ni 52 na chama kilifanikiwa kushinda kesi 47 na kesi 31 bado zinaendelea katika mahakama mbalimbali.

Alisema mwaka 2018, chama hicho kilisimamia suala la watumishi waliosimamishwa kazi kwa kuwa na elimu ya darasa la saba na wote walirudishwa kazini.

Vilevile, alisema tangu uongozi wao uingie madarakani Septemba, 2016 ulikuta ujenzi wa kitega uchumi unaendelea na sasa upo katika hatua za ukamilikaji.

Mtima alisema pia mwaka 2019 chama kwa kushirikiana na Shirikisho la Wafanyakazi (TUCTA) walipigania kurudishwa kwa kikokotoo cha awali na hatimaye wanachama wao kustaafu na kulipwa kwa kanuni za awali.

"Hivyo, ninapenda ieleweke kwamba wanachama wetu wananufaika na mambo mengi zikiwamo fulana na kofia zinazotolewa katika sherehe za wafanyakazi, Mei Mosi kila mwaka," alisema Mtima.

Alisema kila mwezi chama hicho kimekuwa kikipeleka fedha za uendeshaji wa ofisi za mikoa na ruzuku za matawi na kwamba hadi kufikia Machi, mwaka huu, kina wanachama 71,948.

Mtima alisema kuwa, kwa mujibu wa sura ya tano ya katiba ya chama hicho toleo la mwaka 2016, vikao vyote vya chama vya kikatiba na kamati ya utendaji taifa hukutana mara nne kwa mwaka na Mkutano Mkuu wa Taifa hufanyika mara mbili ndani ya miaka mitano.

**"Hivyo, ninapenda ieleweke kwamba wanachama wetu wanufaika na mambo mengi zikiwamo fulana na kofia zinazotolewa katika sherehe za wafanyakazi, Mei Mosi kila mwaka," alisema Mtima.**

**TANZANIA MEDICINES AND MEDICAL DEVICES AUTHORITY**

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

**PRE-QUALIFICATION FOR SUPPLIERS OF LABORATORY EQUIPMENT, CHEMICALS, REFERENCE STANDARDS, MEDIA, GLASSWARE, CONSUMABLES, AND MAINTENANCE OF LABORATORY EQUIPMENT FOR FINANCIAL YEAR 2020/2021**

**INVITATION FOR PRE-QUALIFICATION**

**Date: 14th July, 2020**

1. The Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (TMDA) has set aside funds in its budget towards the cost for the Supply of various Laboratory Equipment, Chemicals, Reference Standards and Media, Glassware and Consumables, and Maintenance of Laboratory Equipment and it intends to apply part of the proceeds of this fund for payments under the contracts for which this prequalification is issued. It is expected that invitations to bid will be made in financial year 2020/2021.

2. Pre-qualification will be conducted through the procedures specified in Regulation 119 of the Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant Services and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations– Government Notice 446 of 2013, and is open to all firms and voluntarily formed joint ventures.

3. TMDA now invites sealed proposals for Pre-qualification of Suppliers and Service Providers in the following categories:-

| LOT No. | DESCRIPTION |
|---|---|
| 1 | Suppliers of Laboratory Equipment |
| 2 | Suppliers of Laboratory Chemicals |
| 3 | Suppliers of Laboratory Reference Standards and Media |
| 4 | Suppliers of Laboratory Glassware and Consumables |
| 5 | Service Providers for Provision of Preventive Maintenance of Laboratory Equipment |

The prospective Suppliers and Service Providers may submit the Pre-qualification Document for one or more Lots.

4. Interested applicants may obtain further information from and inspect the Pre-qualification document at the Office of the Secretary, Tanzania Medicines and Medical Devices Authority Tender Board, 1st floor, Room No. 27, P.O. Box 77150, Off Mandela Road - Mabibo, Dar-es-Salaam, Tanzania, Tel.2450512/2450751, Fax 2450793 from 0900 – 1530 hours local time on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

5. A complete set of the Prequalification document may be obtained from the above mentioned office any interested eligible tenderer and will be evaluated upon payment of a non-refundable fee of Tanzanian Shillings Thirty Thousand Only (TZS 30,000.00). The method of payment should be GePG after collecting the respective control number.

6. Applications for Pre-qualification should be submitted in one original plus one copy in sealed envelopes delivered to the Secretary either by hand or be sent by registered post so as to reach the Secretary, through the address in para 4 above at/before 1400 hours local time on Tuesday 28th July, 2020 and be clearly marked Pre-qualification for Suppliers of respective Lot (s) for the year 2020/2021. Tenders sent by post must be registered.

7. Application for Pre-qualification in form of Telegraphic, Telex, Telefax and e-mail will not be accepted and those which will not be received and not opened in public at the public bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**ACTING DIRECTOR GENERAL**
**TANZANIA MEDICINES AND MEDICAL DEVICES AUTHORITY**

215809501

# ‘Huduma afya ya msingi yashuka hofu ya corona’

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

HOFU ya ugonjwa wa virusi vya corona imesababisha kiwango cha utolewaji wa afya ya msingi kama afya ya uzazi, mama na mtoto na magonjwa mengine ikiwamo malaria na kisukari kwenye maeneo ya kutolea huduma, kushuka.

Hayo yamebainishwa mkoani hapa wakati waandishi wa habari wakijengewa uwezo na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ili waweze kuandika habari zitakazosaidia kuondoa hofu hiyo upande wa wananchi kufuata huduma za afya.

Ofisa programu elimu ya afya kwa umma kutoka wizara hiyo, Meshark Chinyuli, alisema kwa mwenendo wa taarifa zilizo kusanywa zinaonyesha kushuka kwa utolewaji huduma hizo hasa upande wa mama na mtoto kwa kuwa kwa kipindi cha miezi mitatu, wazazi wamepunguza kasi ya kupeleka watoto kupata chanjo na huduma zingine.

Alisema chanjo wanazopatiwa watoto zina umuhimu mkubwa, hivyo wazazi waache kuwanyima watoto wao, haki hiyo ambayo kuikosa kunaweza kusababisha uwapo wa magonjwa ambayo awali kabla ya chanjo hizo yalikuwa hatari kama surua na polio.

“Hatujasubiri matokeo yawe mabaya zaidi ndio tuchukue hatua kwa kuwa bado takwimu za kitaifa za kuonyesha upungufu huo hazijatoka japo kiuhalisia tunapoangalia za kila mkoa mmoja mmoja tunaona kuna utofauti na awali,” alisema. Mratibu wa Elimu ya Afya Mkoa wa Kigoma, Abed Michael, alisema mkoa huo umejipanga kuhamasisha jamii kuendelea na maisha ya kawaida katika mambo muhimu huku ikichukua tahadhari na wanakusudia kukutana na makundi mbalimbali yenye ushawishi katika halmashauri zote.



Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Felix Lawrence, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kumpongeza Rais Jphn Magufuli kwa kuteuliwa tena na chama chake, kugombea urais kwa awamu ya pili pamoja na utendaji kazi wake kwa kuimarisha uchumi wa nchi. Kulia ni mmoja wa viongozi wa serikali hiyo, Bibiana Ngutu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tabora kunufaika umeme gridi ya taifa

**Na Welingtone Masele, SIKONGE**

SERIKALI kupitia Shirika la Umeme nchini (TANESCO), imeanza ujenzi wa njia kubwa ya umeme wa gridi ya taifa yenye msongo wa Kilovoti 132 kutoka mkoani Tabora hadi Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi utakaowezesha wananchi wa mkoa huo kupata umeme wa uhakika.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema hayo alipotembelea ujenzi wa moja ya kituo cha kupozea umeme kinachojengwa katika kijiji cha Ipole, wilayani Sikonge.

Alisema mradi huo utakapokamilika utagharimu Sh. bilioni 70 hatua itakayorahisisha shughuli za uzalishaji na kupunguza gharama ya upatikanaji wa nishati hiyo kwa wananchi wa mikoa hiyo.

Pia, aliiagiza TANESCO kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati kama serikali inavyoelekeza, kwa kuwa tayari fedha za ujenzi huo zipo.

“Huu mradi utakapokamilika utanufaisha wakazi wengi katika mikoa hii miwili kwa kuwa wengi wataanzisha biashara mbalimbali ikiwamo saluni za kunyoa nywele, viwanda vidogo vidogo kama mashine za kusaga na kukoboa nafaka,” alisema.

Naye Msimamizi wa mradi huo kutoka TANESCO, Mhandisi Neema Mushi, alisema mradi huo unajengwa na shirika hilo kwa kushirikiana na kampuni tanzu ya ITIDICO.

Alisema hatua za awali za ujenzi zimeshaanza kwa kujenga vituo vinne vya kupokea na kupoza umeme na kituo kimoja kitapokea na kusambaza umeme wa msongo wa kilovoti 28.

Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Sikonge watakaonufaika na ujenzi wa kituo kitakachojengwa katika wilaya hiyo waliipongeza serikali kwa kuwaletea mradi huo mkubwa utakaounganishwa kwenye gridi ya taifa kwa kusema watakuwa na umeme wa uhakika utakaosaidia kuendesha viwanda vinavyotarajiwa kujengwa katika maeneo yao, huku wakiomba wawekezaji kujitokeza kujenga viwanda ikiwamo cha kuchakata asali kutokana na wilaya hiyo kuzalisha zao hilo kwa wingi.

# Bilioni 71.5/- zatolewa mikopo kilimo biashara

**Na Mwandishi Wetu**

KILIMO biashara nchini kinaendeshwa kwa kiwango kikubwa kupitia uwezeshaji wa asasi inayoitwa Private Agricultural Sector Support (PASS) Trust, Mkurugenzi wake, Nicomed Bohay, anasema.

Katika kipindi cha wiki mbili zilizopita, asasi hiyo imekuwa ikiwakutanisha viongozi na wadau mbalimbali nchini kuzungumzia mipango mikakati ya kuinua wajasiriamali ambao wanahitaji uwezesho wa kifedha.

“Kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu, tumewezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 71.5 tukitumaini kuwa wajasiriamali kupitia kilimo biashara watashiriki zaidi na kuongeza uzalishaji wa bidhaa, alisema Bohay jijini Mbeya.

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, PASS imekuwa na mchango mkubwa katika uchumi na kilimo, ikisaidia wajasiriamali kunufaika na mikopo kutoka taasisi za fedha, sasa wakishirikiana na taasisi 16 zikiwamo benki.

Alisema wajasirimali wanawake wana manufaa zaidi wakipata asilimia kati ya 60 na 80 ya udhamini wa PASS katika mikopo ya benki wakiwa kwenye ama vikundi vya wakulima au mkulima mmoja mmoja.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, PASS hutoa huduma za maendeleo ya kibiashara kama vile tathmini ya mradi, maendeleo ya biashara na kutoa mafunzo kwa makundi ya wakulima.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliipongeza asasi hiyo kwa kazi nzuri inayoifanya katika kuwawezesha wakulima kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.

“Wajasiriamali katika mkoa huu wachangamkie fursa hii ya huduma za PASS kuboresha maisha yao. PASS imerahisisha njia kwa kila mmoja hasa vijana kujihusisha na kilimobiashara na kutengeneza ajira,” alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, aliwataka maofisa kilimo kuhakikisha wanashirikiana na wakulima na kuwapa taarifa kuhusu mikopo hiyo inayowezeshwa na PASS.

**“Kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu, tumewezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 71.5 tukitumaini kuwa wajasiriamali kupitia kilimo biashara watashiriki zaidi na kuongeza uzalishaji wa bidhaa, alisema Bohay jijini Mbeya.**

HABARI KITAIFA

# JWTZ yaikabidhi MORUWASA mabwawa manne

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

JESHI la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kupitia kampuni yake ya Mzinga Holding imeikabidhi mamlaka ya majisafi na majitaka Manispaa ya Morogoro (MORUWASA) mabwawa manne ya maji machafu, baada ya kuyafanyia marekebisho.

Msaada huo ni sehemu ya hatua mbalimbali za kupunguza tatizo la majitaka katika Mkoa wa Morogoro.

Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki ambapo akikabidhi mabwawa hayo, Mkurugenzi Mwendeshaji Mzinga Holding, Meja Idd Nkungu, alisema hatua hiyo ni miongoni mwa majukumu ya JWTZ na kwamba wapo tayari kwa kufanya majukumu ya kijamii muda wote.

Alisema jeshi hilo haliwezi kuvumilia kuona Watanzania wakiendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali bila kupatiwa ufumbuzi kwani kufanya hivyo itatoa taswira mbaya kwa kushindwa kuwa wazalendo.

"Jeshi la Wananchi lipo tayari kutekeleza majukumu yote ambayo pengine yanaonekana yameshindikana... sisi ni wazalendo wa kweli pale mnapoona jeshi linahitajika kusaidia mtuambie tutatatua hizo changamoto," alisema Meja Mkungu.

Akizungumza baada ya kupokea mabwawa hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Mhandisi Tamimu Katakweba, alisema kuwa mabwawa hayo ya majitaka yamekaa zaidi ya miaka 10 bila kufanyiwa ukarabati, jambo ambalo linasababisha kujaa taka.

Alisema kupatikana kwa mabwawa hayo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza athari za magonjwa ya mlipuko, ambazo zingeweza kutokea kama jitihada za haraka zisingechukuliwa katika kukarabati mabwawa hayo.

"Haya mabwawa yalisafishwa mara ya mwisho miaka kumi iliyopita, ni kweli yalikuwa yameshakufa hayafai kutumika tena... lakini tunawashukuru sawa wenzetu Jeshi la Wananchi, hii itasaidia kutunza mazingira katika mkoa wetu," alisema Katakweba.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Dk. Tito Kagize, alitoa wito kwa wananchi kutumia vizuri mabwawa ya majitaka ili kuepukana na adha ya magonjwa ya mlipuko na kuwataka kutumia sheria zinazosimamia mazingira kwa ajili ya kutunza miundombinu ya majitaka.

# Wakulima kahawa wapewa siri ya ongezeko la mavuno

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

WAKULIMA wa kahawa mkoani Kagera wametakiwa kuonyesha ushirikiano kwa wataalamu wa kilimo wanapofika shambani kutoa elimu ya ufufuaji mashamba na upandaji miche bora, ili kuleta tija kwa zao hilo.

Imeelezwa kuwa ushirikiano huo kati ya mkulima na mtaalamu utasaidia ongezeko la mavuno kwani kumekuwapo changamoto za uzalishaji unaosababisha mavuno kidogo ya kahawa tofauti na matarajio ya mkulima.

Hayo yalielezwa na baadhi ya wataalamu wa kilimo katika wilaya za mkoa huo, ambao walipatiwa mafunzo ya ujuzi wa kushawishi mkulima kujifunza kupitia mashamba darasa.

Elizabeth Ndaba kutoka wilayani Kyerwa, alisema kwa kiwango kikubwa wakulima wamekuwa wakitegemea kilimo cha kahawa kama sehemu ya kupata uchumi.

Alisema tatizo linalowakumba ni kutokuwa na elimu ya ufahamu wa kutunza shina la mbuni wa kahawa, ambao unategemewa kwa uvunaji na kwamba kupitia wataalamu, wataonyesha mabadiliko kwa kukubali kushiriki katika elimu ya vitendo.

"Kinachoangaliwa hapa kwenye mafunzo ni kusaidia mkulima kwa kuonyesha vitendo vya ushiriki namna ya kuandaa na kupanda hadi kutunza mche wenye tija, unatarajiwa kuwa na mavuno mengi," alisema Ndama.

Silaji Ismail kutoka Wilaya ya Missenyi, alisema ili kuleta mabadiliko yanayotazamiwa kwa mkulima na kufufua zao la kahawa, vijana mijini na vijiji wajitoe kwa kuelimisha wakulima.

Alisema mwaka 2016 mibuni ilipata ugonjwa wa manjano (mnyauko) ulisababisha baadhi ya wakulima kuendelea na kilimo hicho, ingawa waliendelea kuwa tegemezi kutokana na kushindwa kujipatia kipato kwa ajili ya familia.

Meneja Mradi wa Café Africa mkoani Kagera, Daniel Mwakalinga, alisema uzingatiaji wa elimu ya mashamba darasa yatakayotumika kufundishia mkulima ili kujua namna ya uchipulishaji wa mashamba yao tija kwa mkulima itaongezeka.

Aliongeza kuwa wataalamu ngazi ya kata, wilaya na wakulima kupitia vyama vikuu vya ushirika Kagera Coperative Union 1990LTD (KCU) na Karagwe Distric Cooperative Union (KDCU) watashiriki kusaidia mkulima kuongeza uzalishaji wa tija.

Alisema kipindi hiki cha wakulima wanatakiwa kwenye mavuno na kwamba mradi umeanda wataalamu 40 wenye uwezo wa kutoa elimu ya kutatua changamoto ya mashamba.



Mshtakiwa ambaye ni mganga wa kienyeji mkazi wa Bigabilo, Amri Issa (50) akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Wilaya ya Kigoma, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 jela au faini ya Sh. milioni 4. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Mganga wa kienyeji jela kukutwa na nyara

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma imemhukumu mganga wa kienyeji mkazi wa Bigabilo Amri Issa (50), kutumikia kifungo cha miaka 20 jela au faini ya Sh. milioni 4 kwa kosa la kukutwa na pembe mbili za mnyamapori aina ya kongoni.

Pembe hizo zina thamani ya Sh. 1,557,400, mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na kibali cha mkurugenzi wa wanyamapori.

Mshtakiwa huyo alishindwa kulipa faini hiyo na kupelekwa katika Gereza la Bangwe lililopo Kata ya Bangwe Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Mwakitalu alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na waganga wa kienyeji wengine wenye tabia kama yake.

Alisema upande wa mashaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, alipeleka mahakamani mashahidi 5 na vielelezo vitatu, ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa na pembe mbili za kongoni kinyume cha sheria.

Hakimu Mwakitalu alisema upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote, hivyo mshtakiwa umetiwa hatiani.

Mshtakiwa huyo alijitetea hapo mahakamani kuwa yeye ni mgonjwa wa tumbo pia ana watoto yatima wanamtegemea.

Hakimu Mwakitalu alitupilia mbali utetezi huo na kusema mshtakiwa atakwenda jela miaka 20 au kulipa faini ya Sh. milioni 4 ili iwe fundisho kwake na kwa waganga wa kienyeji wengine wenye tabia ya kuweka nyara za serikali nyumbani mwao bila kuwa na kibali cha mkurugenzi wa wanyamapori.

# CRDB yazindua mfumo wa Qr Code

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

BENKI ya CRDB imezindua mfumo wa kimtandao wa ukusanyaji na utoaji maoni Qr Code utakaomwezesha mteja kutoa maoni yake moja kwa moja hadi ngazi husika kupitia simu ya mkononi (simu janja).

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Kitengo cha Mtandao wa Matawi, Bonaventura Paulo, wakati wa uzinduzi kwa ngazi ya mikoani uliofanyika katika Benki ya CRDB Mwanza.

Alisema mfumo huo utawezesha mteja kupata urahisi wa kufikisha maoni yake kwa ngazi husika muda huohuo pasipo kupitia kwenye mikono ya mtu.

"Tupo hapa kuzindua kampeni ya kukusanya maoni kwa mfumo wa kidigitali mwanzo tulikuwa tunatumia maboksi ya maoni ambao ulikuwa unachukua muda mrefu kufika katika eneo husika, lakini sasa mfumo huu itasaidia kutoa maoni na mrejesho wa maoni ya mteja kwa muda mfupi," alisema Paulo.

Aliongeza kuwa mfumo huo utamsaidia mteja kutoa maoni yake juu ya tawi lingine na utarahisisha kupokea maoni, maboresho, malalamiko na kushughulikia changamoto kwa wakati ili kuongeza ufanisi ili aweze kufarahia huduma za CRDB sambamba na kupata huduma zingine.

Naye Yolanda Uriyo, Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, alisema lengo lao ni kuhakikisha wateja wanapata huduma iliyoborana inayotakiwa hivyo kila mara wataendelea kuboresha namna ya kuendelea kupokea maoni kutoka kwa wateja wanaotumia simu janja kwani mfumo huo ni rahisi na waharaka zaidi.

"Namna ya kutoa maoni unafungua camera unaielekeza palipo na bango la Qr Code moja kwa moja itakupeleka katika tovuti ya maoni ya wateja wetu na hapo unaweza kuchagua tawi ambalo unataka kutoa maoni, hakika huduma hii italeta mabadiliko makubwa na hakutakuwa na ucheleweshaji wa utoaji majibu," alieleza Uriyo.

Naye Meneja wa CRDB Kanda ya Ziwa, Lusingi Sitta, alisema kutokana na thamani kubwa walionayo wateja wao wanapaswa kuchangamkia fursa na kuiona huduma hiyo ni yao kwani itawasaidia kupata ufumbuzi wa changamoto zao kwa wakati mwafaka.

**"Tupo hapa kuzindua kampeni ya kukusanya maoni kwa mfumo wa kidigitali mwanzo tulikuwa tunatumia maboksi ya maoni ambao ulikuwa unachukua muda mrefu kufika katika eneo husika, lakini sasa mfumo...**

# RC Tabora awatumia salamu wanaolima, kuchungia hifadhini

**Na Wellingtone Masele, KALIUA**

MKUU mpya wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amewataka viongozi na watumishi ambao wamekuwa wakichochea baadhi ya wakulima na wafugaji kuingia katika maeneo ya hifadhi na kufanya shughuli za kiuchumi kuacha mara moja.

Alitoa agizo hilo alipokuwa katika ziara ya kutembelea miradi ya maendeleo wilayani Kaliua, alionya kuwa mtu yeyote anayevamia misitu ya hifadhi na kuishi au kufanya shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, ufugaji nyuki anaenda kinyume cha sheria za nchi.

Alisema kuwa serikali ilishatoa maelekezo ya maeneo yaliyoruhusiwa kukaliwa na wananchi na kufanya shughuli za kiuchumi, hivyo yeyote aliyevamia maeneo yasiyoruhusiwa kinyume na utaratibu anapaswa kuondoka mara moja.

RC alibainisha kuwa Kamati Maalumu iliyopewa kazi na Rais John Magufuli ilipita katika halmashauri zote na kubainisha maeneo yote yaliyovamiwa, ambapo ilibainisha wazi kuwa baadhi ya watu wanaoishi katika maeneo hayo wamekuwa wakisababisha uharibifu mkubwa wa rasilimali zilizopo katika hifadhi hizo.

Aliongeza kuwa mbali na uharibifu huo pia wamekuwa wakisababisha uvunjifu wa amani ikiwamo kushambulia askari wa wanyamapori wanaolinda hifadhi hizo.

Aidha, aliwataka wanaojihusisha na vitendo vya mauaji ya watu wasio na hatia katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo kutokana na imani za kishirikina, wivu wa kimapenzi na ugomvi wa mali kuacha mara moja vitendo hivyo, vinginevyo watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Michael Nyahinga, alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa halmashauri hiyo imeanzisha mfumo wa elimu ya kujitegemea ambao huwezesha wanafunzi kushiriki kazi za mikono baada ya muda wa masomo.

Alisema kuwa baadhi ya kazi zinazofanyika ni ufyatuaji tofali ambazo hutumika kujengea vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo, hivyo kupunguza changamoto ya upungufu wa miundombinu uliopo kwa sasa.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Waama, Kata ya Gisambalag wilayani Hanang' mkoani Manyara, Martin Gurtu (kushoto), akionyesha jana sehemu ya barua walizotuma kwenda katika ofisi mbalimbali za serikali kuomba kutatuliwa kwa mgogoro wa mipaka ya kijiji ulioduma kwa zaidi ya miaka 23. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamwomba JPM kusaidia utatuzi mgogoro wa ardhi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAKAZI wa Kijiji cha Waama Kata ya Gisambalag wilayani Hanang' mkoani Manyara, wamemwomba Rais John Magufuli kuingilia kati ili kutatua mgogoro wa mipaka kati yao na kijiji jirani cha Dirma, ulioduma kwa zaidi ya miaka 23.

Ombi hilo lilitolewa juzi jijini Dodoma na Mwenyekiti wa Kijiji cha hicho, Martin Gurtu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Mwenyekiti huyo pia alikwenda jijini Dodoma wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kupata fursa ya kuwaona viongozi wakuu wa nchi na kuwafikishia kilio hicho.

Gurtu alisema kuwa pamoja na jitihada zake za kuja jijini Dodoma, lakini amekosa fursa ya kumpata Rais ili amfikishie kilio chao cha muda mrefu.

"Mgogoro huu kwetu umekuwa kero kubwa sana, kila siku wakulima na wafugaji wanapigana kutoka tu na mpaka uliopo kuwekwa bila ya kuwapo kwa maridhiano ya pande zote mbili," alisema Gurtu.

Pia alifafanua kuwa ombi lao kubwa ni kupata mpaka wenye maridhiano ambao utaheshimiwa na kila mtu kwani ulipo hivi sasa haukuhusisha vijiji vyote viwili.

Alisema kutoka na tatizo hilo, kumekuwa na matukio ambayo yamekuwa yakitokea ikiwamo mazao ya wakulima zaidi ya hekari 3,000 mwaka 2008 yalifyekwa pamoja na nyumba zaidi ya 67 kubomolewa.

Aliongeza kuwa pamoja na matukio yote hayo hakuna hatua iliyochukuliwa na serikali hali ambayo inawatia shaka kuwa ipo siku machafuko yanaweza kutokea.


Vile vile, alisema katika kipindi hicho chote cha miaka 23, wamekuwa wakizunguka kila eneo ili kupata haki yao lakini hakuna mafanikio.

"Tumekuwa tukizunguka kila sehemu katika ngazi mbalimbali za serikali, akiwamo mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya pamoja na kupeleka barua zetu kwa mawaziri akiwamo waziri wa ardhi, lakini mpaka sasa hali bado ni mbaya," alifafanua Gurtu.

Kwa mujibu wa barua iliyoandikwa na msaidizi wa mkuu wa mkoa wa Manyara kujibu malalamiko ya wananchi hao ya Juni 19, 2020, yenye kumbukumbu namba FA.33/347/01"F"/17, mipaka iliyopo ipo kwa mujibu wa sheria na kuwataka wananchi hao kuendelea kuiheshimu.

"Mipaka iliyopo iliwekwa kwa mujibu wa sheria na iliwekwa wakati Waama ilikuwa miongoni wa kitongoji kilichounda kijiji cha Gisambalag na kwa kipindi chote hapakuwahi kutokea mgogoro baina ya Dirma na Gisambalag," ilieleza sehemu ya barua hiyo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 14, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


Ukurasa 13
**Matokeo jamii inapochoka watoto 'kusota' chini ya miti**


Ukurasa 12
**Inahitajika hamasa kilimo DSM, mvua miezi 8 yaneemesha mapori**


Ukurasa 14
Wanasayansi na tahadhari binadamu wanavyoangamia

SAYANSI

NA MICHAEL ENEZA

# Kitendawili cha COVID-19 virusi vinavyoibuka inapotimu miaka

WAKATI baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam na hata kwingineko nchini ingawa hali zao inatofautiana wanaanza kusahau woga waliokuwa nao wa baa la corona, hali inaendelea kuwa tete katika nchi nyingi duniani. Jitihada za kufungua shughuli za kawaida zikichuliwa lakini tahadhari zinazozingatiwa hazijawa na mafanikio kama Tanzania na baadhi ya nchi za Afrika zilizokuwa na maambukizi hafifu ya virusi vya corona.

Katika mataifa mengine juhudi za kufungua njia za uchumi zimekuwa kichocheo cha kupanda kwa kasi maambukizi, tofauti na ilivyo hapa Tanzania na siyo rahisi kutaja sababu ya tofauti kama hizo, labda kwa kuangalia historia ili kupata picha ya tukio hili.

Hili ni eneo mojawapo ambalo wataalamu huenda wanapata kigugumizi kulizungumzia kwani haliendani na elimu ya takwimu kwa mfano kuhusu magonjwa, kuwa magonjwa hayawezi kuzuka kwa vipindi vinavyotabirika, au maradhi kujirudia kwa kipindi maalum.

Suala la kushangaza la COVID-19 ni kuwa ndicho kilichotokea, kuwa homa ya mapafu inayoitwa Spanish Influenza ilianza kuenea nchini Hispania na Ureno iliyozuka mwaka 1919 na kudumu kwa miaka mingi.

Historia inaonyesha kuwa iliua watu milioni 50 kote duniani na katika Bara la Afrika ilisambaa kwa kiasi baada ya vita kuu vya kwanza vya dunia, ila linalokumbukwa ni kwamba bara hilo lilipoteza watu milioni 2.5. Bado hakuna uwezo wa kulinganisha kufariki kwa watu wakati huo na katika janga la COVID-19 hivi sasa kwa sababu siyo rahisi kupata picha ya dawa zilizotumiwa kwa wakati huo.


Karibu dunia nzima watu wamelazimika kuvaa barakoa kuepuka maambukizo. **PICHA: MTANDAO**

Ila kwa kulinganisha unawezekana kuwa nyingi kati ya dawa za kila siku za hospitalini ambazo baadhi zimetumika kutibu watu wenye maambukizi hafifu ya COVID-19 hazikuwapo na zimetengenezwa katika kipindi kilichofuata au kuanza kusambaa duniani.

Ila kama walikuwa na ufahamu wa dawa za miti, hizo zilikuwapo siku zote na huenda pia zilisaidia kuponya wengi.

Hivyo, kuna tatizo la kufuatana kwa janga la corona kutoka mwaka 1919 na kuzuka tena ugonjwa kama huo halafu kwa mapana hayo hayo mwaka 2019.

Hata kama ulianzia China na siyo Hispania kama awali. Kama ni ugonjwa peke yake, kwa maana ya mfumuko wa virusi kutoka kwa mnyama vilipogusa ngozi ya binadamu, au kuingia mwilini endapo nyama hiyo haikuiva vizuri, iweje uwe na mfuatano wa miaka 100 kamili?

Halafu mfuatano huo unaleta hisia ya kuwapo na mwingine wa kuwapo maradhi kama hayo mathalani influenza ya karne iliyopita ilivyoendelea kwa muda mrefu na kuvuruga uchumi duniani COVID-19 pia ina mwelekeo huo.

Kilicholeta wakati huo ni uchumi wa dunia kuvurugika haikuwa kukosekana kwa kazi za kufanya ila kukata tamaa kwa watu wengi, baada ya watu milioni 40 kuwa wameshapoteza maisha, miaka 10 baadaye, 1929. Ndiyo kilianza kipindi kilichoitwa cha mdororo mkuu wa uchumi au great depression, kilichodumu hadi mwaka 1932 ambako Marekani iliingia katika mwelekeo wa sera ulioitwa 'makubaliano au agano jipya 'new deal,' kati ya watu na serikali kuhusu uwezeshaji kiuchumi.

Suala ni jinsi gani mdororo wa uchumi ambao umeanza kuenea duniani kutokana na COVID-19 utaipeleka dunia katika 'makubaliano mapya' ya kiuchumi ili maradhi hayo yaishe ndicho kinachosubiriwa.

Dhana hiyo ni mfuatano mwingine ambao unawezekana kihesabu, kuwa kutokana na kufuatana miaka 100 kwa corona ya mwanzo wa karne iliyopita na hii ya mwanzo wa karne ya 21, huenda kuna uwezekano kuwa vipengele vya mfumuko wa Spanish Influenza na corona ya sasa vitafanana.

Dhana hiyo ina umuhimu kiasi fulani kwa sababu inaondoa 'ukungu' au 'utando wa buibui' katika mijadala ya mwelekeo wa uchumi duniani katika mazingira ya maradhi hayo, kuondoa kigezo cha kufananisha na vita kuu vya pili . Havifanani.

Wataalamu wengi zaidi huko ng'ambo wanapenda kufananisha kipindi hiki na vita vya pili kwani nchi za Magharibi zilishinda na baada ya hapo makubaliano mapya ya Marekani yalianza kutumia nchi za Ulaya ili kuondoa hitilafu za kimfumo yaliyofikisha mataifa hayo katika vita, hasa Ujerumani na Ufaransa, na kusaidia Uingereza kuinua tena uchumi wa kiraia, si kuzalisha silaha.

Kutaka kutumia mfano huo kwa janga la COVID-19 ni kumalizia 'new deal' bila kianzio cha aina hiyo. Halafu mwaka 1945 kisayansi ni wakati wa viwanda vya ajira nyingi, wakati corona inachochea kuweka kwenye mashine-kazi ili bei zipungue na viwanda visife.

Wataalamu wana kazi mbele yao, yaani kupambana na COVID-19 wakipanga kutoka kwa utaratibu wa kuinua uchumi si kutafakari vifo vya mamilioni ya watu kwani kuna dalili kuwa corona haitamalizika kipindi cha joto katika nchi za Ulaya na Marekani.

Misitu ya Brazil ina joto mwaka mzima lakini corona inaangamiza makabila yaliyojificha ndani kabisa ya misitu hiyo.

Endapo majira ya baridi yatafikiwa halafu jitihada za chanjo nazo hazitaweza kuleta majibu chanya kama ilivyokuwa kwenye dawa za 'hydroxyl-chloroquine' aliyoipigia chapuo Rais Donald Trump, ambayo haitibu, labda ni mitishamba itakayosaidia, ila inafaa tu kwa kupunguza matatizo mepesi siyo mapafu yanapotoboka na damu kuganda sehemu mbalimbali za mwili.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Hitaji la hamasa kilimo Dar, mvua miezi 8 yaneemesha mapori

WATAZANIA wengi huenda wameanza kuelewa masuala ya mabadiliko ya tabianchi, lakini kuna uwezekano kuwa hawayatilii maanani, licha ya kuyazungumzia na kuyafuatilia.

Kinachoonekana kuwa hakijafanyika ni kuchukua hatua kukabiliana na mabadiliko hayo na kujua kuwa kila kunapokuwa na mabadiliko chanya ni lazima kufanya jambo.

Mabadiliko ya tabianchi ni matokeo ya kubadilika kwa hali ya hewa kunakoletwa na ongezeko la joto duniani kutokana na kuharibu anga za juu ambazo zinasababisha mionzi mikali ya jua kupenya na kuifika duniani.

Huenda wengi wanaamini kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi zinamhusu mkulima au mfugaji zaidi kwa vile ndiye anayetegemea ardhi na mvua, bila kujua kuwa madhara yapo kwa kila binadamu.

Athari hizi zinawagusa wote kwa kuwa joto na fukuto kali mathalani, hukausha maji mwilini na kuongeza uwezekano wa kuwa na maradhi ya kuwa na mawe kwenye figo, kupata magonjwa ya ngozi hata saratani inayotokana na kupenya kwenye ngozi mionzi mikali ya jua maarufu kama ultra violet rays (UVA).

Mabadiliko ya tabianchi yanawalazimu wengi kubadilika na kuona kuwa ni zama za kuchukua hatua kulingana na misimu ikiwa na mvua watu kulima na kufuga zaidi pamoja na kutunza maji.

### KUPUUZA MVUA

Kuanzia Oktoba mwaka 2019 hadi Oktoba 2020, mvua ilinyesha kiasi cha kutosha na katika mikoa mingi ikiwamo Dar es Salaam.

Utafiti uliofanywa na Nipashe sehemu mbalimbali Dar es Salaam, wakati wa kipindi hicho, unadhihirisha kuwa watu hawajabadilika kifikra na wala hawathamini mvua hasa kuitumia kwa kilimo.

Mvua iliyoanza Oktoba hadi Mei 2020, ikinyesha miezi nane ni msimu ambao masika na vuli viliungana, lakini licha ya kunyesha huko, watu wengi Dar es Salaam hawakuwa na hamasa ya kujishughulisha na kilimo. Nipashe ilitembelea maeneo mengi kama Madale, Msumi, Makabe, Kibamba, Kiluvyia na Kibaha na kugundua kuwa kuna sehemu nyingi zenye mashamba na viwanja ambavyo havijajengwa.

Japo watu walishuhudia mvua kwa karibu mwaka mzima, watu hawakujishughulisha na kulima mahindi, kunde, mihogo, mabogo na mazao mengine yanayostawi ukanda huo.

Pengine mvua ya miezi nane ambayo ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi, ilitegemewa kuwa fursa ya kupanda mihogo, viazi, mbaazi, migomba na matunda hasa mapapai lakini hakuna jitihada za kutosha za kusafisha vichaka ambavyo baada ya mvua vimezidi kuimarika na kuwa makazi ya wanyama na wadudu.



Athari za wadudu waharibifu wa mazao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Ni kweli ni lazima kutumia mbolea kama DAP kupandia, lakini pia za kukuzia na 'booster' ambayo ni mbolea ya majani na CAN kuzalisha na kuimarisha mbegu.



Wakazi wengi wa Dar na mikoa mingi nchini tangu Mei hadi mwezi huu wanalalamikia upepo mkali ambao unakausha maji kwenye madimbwi, mazao hasa matunda, unavunja miti na kusababisha vumbi kujaa ndani ya nyumba.

Baada ya mvua ya miezi nane sasa ni upepo wa takriabni miezi mitatu ukivuma mchana na usiku, lakini maghala yao hayana akiba ya chakula wala maji.

Huenda wakazi wa Dar es Salaam wanakosa wahamasishaji, hivyo ni wakati wa kuamua namna ya kuhamasisha watu kutumia mapori na kulima chakula wakati wa mvua.

Mazungumzo na baadhi ya wakazi wa Dar yanaonyesha kuwa wanafahamu kuwa kuna mabadiliko lakini wanakosa hamasa ya kuhimiza kilimo.

Jimmy Mbajo, anayeishi Madale anasema kilimo Dar kina changamoto nyingi kama ongezeko la wadudu wanaoshambulia mapapai, mboga, mastafeli na mapera lakini hakuna maofisa ugani wanaowapa ufumbuzi na kuwahamasisha kulima.

"Kuna panzi na funza wengi wanashambulia mahindi. Mhindi ukichipuka unashambuliwa. Unaweza kupanda lakini ikiwa kazi ngumu kupata mazao. Ili kuvuna utahitaji kutumia dawa kwa wingi kuua wadudu."

Anazungumzia suala la ukungu na wadudu wanaoibuka na kushambulia mazao kama matunda hasa mapapai na maembe, mapera mboga za majini na kusababisha majani na matunda hayo kuwa myeusi au myeupe kama yamemwagiwa unga au chokaa.

Anasema hali ilivyo kilimo bila viuatilifu na mbolea kwa wingi kinaweza kisifanikiwe na kwamba njia za asili za kuangamiza wadudu kama vile majani yenye dawa ya muarobaini au minyaa au aloivera hazisaidii kuua wadudu hao wakali wanaozaliana kwa kasi zama hizi, ndiyo maana watu huogopa kulima.

Lakini pia, anaeleza kuwa ukame unaleta usugu wa vimelea vinavyosambaza magonjwa kwenye mazao mfano matunda yanashambuliwa na ukurutu mweusi unaosababishwa na fangas. Machungwa, ndimu, maembe na mafenesi ni miongoni mwa mazao yanayopata ukurutu huo ambao wakati mwingine hausikii dawa.

Wakulima wanahisi kuwa licha ya mahindi kuwa chakula kikuu cha Watanzania huenda hayastawi Dar es Salaam, ndiyo maana wanasita kupanda. Wanasema wengi hawalimi kwa sababu wanakosa mahindi licha ya kutumia mbegu za kisasa, mbolea, dawa na nguvu nyingi .

Gazeti hili liliwatembelea wauza mbegu hasa za mahindi sokoni Kariakoo, katika mahojiano wanaeleza kuwa kila ukanda una mbegu zake na pwani zipo za kutosha.

Wauzaji hao wanasema pengine wakati umefika wa kuweka maofisa ugani kwenye ofisi za kata ili kuhamasisha kilimo Dar na pia kuelezea umuhimu wa kutumia mbolea za kupandia na kukuza mahindi.

"Ni kweli ni lazima kutumia mbolea kama DAP kupandia, lakini pia za kukuzia na 'booster' ambayo ni mbolea ya majani na CAN kuzalisha na kuimarisha mbegu. Tusisahau viuatilifu ili kuangamiza visumbufu," anasema Vincent Ngomuo, anayeuza mbegu na pembejeo Kariakoo.

### MVUA ZA KWANZA

Yusufu Msonde, mkazi wa Mitamba mkoani Pwani anasema wakulima hawajahamasika na dhana ya mvua za kwanza ni za kupandia.

"Wanahitaji msukumo mpya mvua zikinyesha ni lazima kupanda bila kujali uko Dar es Salaam au Dakawa. Tuendelee kuamini kuwa mvua za kwanza ni za kupandia si kutayarisha mashamba.

"Mvua ikinyesha tupande tusipoteze wakati tena uwe umeandaa ama hujatayarisha shamba anza kulima, mvua ya miezi nane haikutakiwa kutuacha Wanadar es Salaam na njaa." Anasema mkulima huyo.

Anasema ni wakati kwa wakulima wa Dar kujua kuwa kuna ukame na joto kali hivyo watumie mbinu ya kilimo mchanganyiko mfano wapande mazao ya aina mbalimbali kwenye shamba moja.

"Tuchanganye mihogo, mtama, kunde, mbaazi , mahindi na choroko kwa kuwa hakuna uhakika iwapo mvua itaendelea hadi mwisho wa msimu ama kutakuwa na mabadiliko." Anaongeza Msonde.

ELIMU
## NA SABATO KASIKA

# Matokeo jamii inapochoka watoto ‘kusota’ chini ya miti

KATIKA jitihada zake za kuondoa tabaka la wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliamua kuja na mikakati mbalimbali yenye lengo la kujenga uwiano sawa wa utoaji wa elimu kwa wote.

Moja ya mikakati hiyo ni serikali kugharamia elimumsingi kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne . Aidha, kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), utaratibu unaoanzia chini kwa wanafunzi wa awali hadi shule za msingi, huku ikiagiza kila shule ya msingi kuwa na darasa la wanafunzi wa awali.

Wizara katika msisitizo wake mkubwa ni kuhakikisha nchi inakuwa na Watanzania walioelimika na stadi, maarifa na uwezo wa kutumia elimu walioipata kwa manufaa yao , jamii na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, pamoja na mikakati hiyo, kumekuwapo na changamoto mbalimbali ambazo kama wananchi watajiweka pembeni na kudhani ni jukumu la serikali, yawezekana kusiwe na matokeo chanya kama ilivyotarajiwa.

Miongoni mwa changamoto hizo ni uhaba wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa awali kwenye shule mbalimbali za msingi, hali inayosababisha baadhi yao wasomee chini ya miti.

Wilaya ya Musoma mkoai Mara, ni moja ya maeneo ambayo yanakabiliwa na changamoto hiyo, lakini wazazi wameiona na sasa wameamua kujenga madarasa ya wanafunzi wa awali kwa ajili ya watoto wao.


Baadhi ya wanakijiji wa Karusenyi, wakishirikiana na fundi kujenga darasa la awali kijijini hapo. **PICHA: OFISI YA MKUU WA WILAYA**

### JINSI YA KUSHIRIKI

Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Vincent Anney anasema, kwa sasa katika vijiji mbalimbali, wazazi wanashiriki kwa kusomba maji, mawe, mchanga, kokoto na vitu vingine muhimu kwa ajili ya kufanikisha ujenzi huo.

“Kwanza nitoe ufafanuzi kwamba wilaya ya Musoma ina halmashauri mbili, ambazo ni Mji wa Musoma na Musoma Vijijini ambako ndiko kwenye changamoto ya ukosefu wa madarasa ya awali,” anasema Dk. Anney.

Anasema, kwa sasa kuna shule za awali 11 zinaendelea kujengwa ili kutatua tatizo la watoto madarasa ya awali kusomea chini ya miti au kutembea umbali mrefu kufuata elimu na pia kuondoa mlundikano wa wanafunzi madarasani.

“Baadhi ya madarasa hayo kwa ajili ya shule za awali shikizi ni ya vijiji vya Karusenyi, Kata ya Nyamrandirira, Busamba, Kata ya Etaro, Kamuguruki, Kata ya Nyakatende,” anasema.

Anaeleza, ujenzi huo pia umechangiwa na wadau wa elimu akiwamo Prof. Sospeter Muhongo, ambaye hivi karibuni amechangia mabati 54 kwa kijiji cha Karusenyi na mifuko 100 kwa ajili ya madarasa ya awali ya kijiji Kamguruki.

Anafafanua kuwa mazingira ya kusomea chini ya miti siyo rafiki kwa watoto, na kwamba yanaweza kusababisha washindwe kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, hivyo kuna umuhimu wa kuwandoa huko.

“Kwa mfano wanaweza kuwa wanaendelea na masomo chini ya mti, halafu mvua ikanyesha na kulazimika kukatisha masomo ili kuipisha mvua, hali ambayo kimsingi inakwamisha maendeleo yao kielimu,” anasema Mkuu wa Wilaya.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya anasema, Musoma Vijijini ina vijiji 68 na shule za msingi 111 za serikali, na kwamba wananchi nao wamehamasika na kujitolea nguvukazi zao kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya wanafunzi wa awali.

“Kwa njia hii tunaweza kutimiza lengo la wizara la kuondoa tabaka la wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa vijana na watu wazima kwa kujenga uwiano sawa wa utoaji wa elimu kwa watu wote,” anasema.

Halikadhalika anaongeza kwamba mbali na ujenzi huo, wamekuja na mkakati ya kuinua elimu ya msingi, ambao umesaidia kuifanya ishuke namba moja, katika matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la nne, kati ya wilaya saba za mkoa wa Mara.

### MKAKATI UNAOTUMIKA

Dokta Anneya anasema, uboreshaji wa miundombinu ya shule, upatikanaji wa vifaa muhimu kama madawati, vitabu na mambo mengine muhimu, ni mikakati ambayo sasa imeanza kuzaa matunda.

“Kwa mfano, madawati zaidi ya 10,000 yalishagawiwa katika shule mbalimbali, vitabu vingi vya maktaba vilishasambazwa, madarasa zaidi ya 450 yalishajengwa huku wadau wa elimu wakiendelea kuchangia,” anasema.

Anawasifu, wananchi wa vijiji mbalimbali nao hawako nyuma katika hilo, kwa vile wamedhamiria kuboresha elimu kwenye maeneo yao na wanajitolea kwa hali na mali katika kufanikisha hilo.

“Nalo shirika la kimataifa la PCI kutoka Marekani na Profesa Sospeter Muhongo, wamechangia kwa kiasi kikubwa, katika uboreshaji wa elimu na sasa wanaendelea kuchangia ujenzi wa maktaba na vyoo,” anasema.

Anasema, kwa kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu, wadau hao pamoja na wazazi, wameifanya wilaya ya Musoma kutoka kwenye nafasi ya mwisho na kuwa ya kwanza katika mtihani wa darasa la nne.

“Uboreshaji wa miundombinu ya elimu umeanza kuzaa matunda, kwani shule za Halmashauri ya Musoma zilishika namba moja kwenye mtihani wa taifa wa darasa la nne wa mwaka jana,” anasema.

Anasema wataendelea kushirikiana na wadau wa elimu kuboresha zaidi shule ili kuhakikisha wilaya hiyo inaendelea kushikilia namba moja hata kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

### WAZAZI WANASEMAJE?

Baadhi ya wazazi wanasema, uhamasishaji uliofanywa na wadau wa elimu katika vijiji mbalimbali, umechangia kuwafanya watambue umuhimu wa elimu na hivyo kujitolea nguvukazi yao kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.

Sadick Chiguma ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Suguti, anasema, baadhi ya watu walikuwa wakiamini kwamba uboreshaji wa miundombinu ya shule ni kazi ya serikali na hivyo kujiweka pembeni.

“Lakini bahati wadau wa elimu wametusaidia kuelimisha wananchi wetu, wameelewa na sasa wanashiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za maendeleo, yakiwamo ya elimu,” anasema Chiguma.

Anasema, yeye kama kiongozi, yupo mstari wa mbele kuhimiza wakazi wa kijiji chake kujitolea kuboresha miundombinu ya elimu kwa ajili ya watoto wao ili kusiwe na mtoto asiyejua kusoma na kuandika.

“Kwa mzazi anayejua maana ya elimu, hawezi kukwepa kuchangia maendeleo ya shule kwenye eneo lake, ingawa wapo baadhi wanaodhani kwamba hatua ya serikali kutoa elimu ni tiketi kwao kujiweka pembeni,” anasema.

Mkazi wa Kijiji cha Kusenyi alijejitambulisha kwa jina la Emmy Mkama, anasema, karne hii ya sayansi na teknolojia ni muhimu jamii kuzingatia elimu ikiwa ni pamoja na kuwezesha watoto kusoma.

“Katika hili, mzazi na mlezi anatakiwa kushiriki kuanzia kuandikisha watoto shule, kufuatilia maendeleo yao na pia kujitolea kuboresha miundombinu ya shule badala ya kuiachia serikali pekee,” anasema Emmy.

> Kwa mfano, madawati zaidi ya 10,000 yalishagawiwa katika shule mbalimbali, vitabu vingi vya maktaba vilishasambazwa, madarasa zaidi ya 450 yalishajengwa.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Wanasayansi na tahadhari binadamu wanavyoangamia



Ndivyo wanasayansi wanavyoona madaraja kubomoka na kuwa mapori. **PICHA: MTANDAO**

WANASAYANSI wanaona kuwa ushawishi wa binadamu duniani umefikia kiwango ambacho kinamtishia yeye mwenyewe.

Wanadamu wameathiri kwa njia nyingi mazingira, kutoka moto hadi kilimo, lakini,wamefikia kiwango cha uchafuzi wa hewa kwenye anga za juu, hadi vipande vya plastiki chini ya bahari na leo haiwezekani kupata mahali duniani ambako binadamu hajapaathiri.

Lakini, kuna wingu jeusi katika upeo wa macho yao mwisho wa mwanadamu hauepukiki, ndivyo wanavyosema wataalamu.

Zaidi ya asilimia 99 ya viumbe ambavyo vimeishi duniani vimeangamia, vingi wakati wa majanga yaliyotokea zama zilizotangulia.

Binadamu hawajawahi kukabiliwa na tukio la kiwango kama hicho , lakini hivi karibuni ama baadaye huenda wakaathiriwa.

### MWISHO HAUEPUKIKI

Kwa wataalam wengi swali si kwamba binadamu wataangamia lakini ni hili watawahi kuangamia na hiyo itakuwa lini?

Na kuna wengine ambao wanafikiria huenda ikawa karibuni wala siyo siku za baadaye.

Mwaka huu 2020, mtaalamu wa masuala ya virusi Frank Fenner, anasema kwamba huenda wakaangamia karne ijayo, kutokana na idadi kubwa ya watu, uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya anga.

Wanasayansi wanatabiri kuwa miji itaangamia, misitu itamea juu ya madaraja na yataanguka Maisha yataendelea na makovu atakayoacha duniani yatapotea kwa haraka .

> “ Madaraka na malipo ya ziada wanayopata wanasiasa wanastahili? Au kuna watu wengine wangefanya majukumu hayo hivyo kutoa fursa za ajira na kipato wa raia au wapigakura wao?

"Miji itaangamia, misitu itamea na madaraja yataanguka. Na baadaye kila kitu kitaoza ", anasema Alan Weisman, mwandishi wa kitabu cha The World Without Us, kilichochapishwa 2007 na ambacho kinaangazia ni nini kitakachofanyika iwapo binadamu atatoweka duniani.

Iwapo hawezi kuvivunja atavizika. Na muda mfupi baadaye, kila kitu kilichoachwa na binadamu kitabadilika na kuwa plastiki.

### USHAHIDI ULIOPO

Katika eneo la maili 19 linalozunguka kiwanda cha umeme cha Chernobyl nchini Ukraine, ambacho kilichafuliwa kufuatia kulipuka kwa kinu cha kinyuklia, mimea na wanyama sasa wanaishi katika sehemu hiyo vizuri zaidi ya ilivyokuwa hapo awali.

"Ushahidi wa haya yote ni kutazama eneo la dunia ambalo tumelazimishwa kuishi.

Utafiti uliofadhiliwa na baraza la utafiti kuhusu mazingira uligundua idadi kubwa ya wanyamapori katika eneo hilo, ikimaanisha kwamba binadamu si hatari kwa mazingira yaliopo ikilinganishwa na miaka 30 ya mionzi mikali."

Kasi ambayo asili au maumbile husimamia mazingira ya eneo fulani inategemea na hali ya anga.

Katika eneo la jangwa la mashariki ya kati uharibifu uliofanywa maelfu ya miaka iliyopita unaonekana, lakini si kwa miji ya miaka 100 iliyopita katika msitu wa tropiki.

### WANYAMA MIJINI

Mwaka 1542, wakati Wazungu walipoona misitu ya mvua nchini Brazil, waligundua miji, barabara na mashamba kandakando ya mito mikubwa.

Hatahivyo, baada ya wakazi kuangamia kutokana na magonjwa yalioletwa na wageni hao miji hiyo ilichukuliwa na wanyama.

Ni wazi kwamba uharibifu wa Las Vegas utaendelea kwa kipindi kirefu ukilinganishwa na ule wa mji wa Bombay. Mimea na wanyama ambao wamekuwa na uhusiano wa karibu na binadamu ndiyo watakaoathirika pakubwa iwapo wanadamu wataangamia.

Mimea inayotumiwa na wanadamu kama chakula ambayo hutegemea dawa za kuuwa wadudu na mbolea itaangamia na badala yake mimea mingine kuchipuka.

"Mimea hiyo itarithiwa kwa haraka", anasema Wiseman. Karoti zitabadilika na kuwa mwitu."

Kutoweka mara moja kwa dawa za kuuwa vidudu kutasababisha ongezeko la wadudu.

Wadudu hutembea , huzaana haraka na kuishi katika mazingira yoyote, na hivyobasi kuwafanya kuonekana kama wanyama wanaoweza kufanikiwa kwa haraka licha ya kwamba binadamu wanajaribu kuwapunguza.

"Magonjwa ya Biblia" ambayo huharibu mimea yatakuwa hatari zaidi utokana na mabadiliko ya anga.

"Yanaweza kuongezeka na kuzoea kwa haraka zaidi ya kitu chochote kile duniani, isipokuwa pengine viini", anaelezea Weisman.

### KULA KITU

Kitu chochote kinachofanana na mlo kitaliwa.

Ongezeko la wadudu badala yake litaongeza idadi ya wanyama wanaowala kama vile, vindege, panya, mjusi na popo huku nao pia wakiongeza idadi ya wanyama wanaowala.

Kitu chochote kinachofanana na mlo kitaliwa. Lakini kila kinachopaa jua lazima kishuke. Idadi kubwa haitaendelea kuishi katika kipindi cha muda mrefu wakati chakula kilichoachwa na wanadamu kitatoweka.

Kuangamia kwa wanadamu kutakuwa na athari katika mtandao wa chakula kwa takriban miaka 100, kabla ya hali mpya ya kawaida kuanza kuonekana.

Baadhi ya ng'ombe mwitu pamoja na kondoo wataendelea kuishi, lakini wengi wao walifugwa kama wanyama wanaokula polepole na wakaidi, hatua itakayowafanya kuangamia kwao kwa idadi kubwa.

"Nadhani punde tu wataliwa na wanyama pori", anasema Weisman.

Paka hufanikiwa pakubwa kila wendapo.Swali la iwapo maisha ya 'kiintelijensia' yataendelea tena ni gumu kujibu.

Nadharia moja kwamba ya 'intelijensia' itaendelea ni kwasababu iliwasaidia mababu zetu kuweza kukabili athari za kimazingira. Iwapo watu wataangamia kesho, itachukua maelfu ya miaka kwa gesi ya kijani iliojaa angani kurudi kama ilivyokuwa kabla ya kuanza kwa viwanda.

"Hali ya anga inabadilika kwa kasi kuu na katika mwelekeo hatari sana:"Imesema ripoti ya wanasayansi inayoonya kuhusu takwimu za viwango vya joto duniani.

### VINU VYA NYUKLIA

Kuna tatizo la vinu vya kinyuklia. Ushahidi wa kinu cha nyuklia cha Chernobyl unaonesha kwamba mazingira yanaweza kujiponya kutokana na mionzi.

Lakini kuna takriban vinu 450 vya kinyuklia duniani ambavyo vitaanza kuyeyuka punde tu mafuta ya majenereta ya vinu hivyo yatakapokwisha. Hakuna njia ya kubaini athari za kuvuja kwa mionzi katika mazingira . Na hilo ni kabla hawajaanza kufikiria kuhusu uchafuzi mwingine wa mazingira.

### MILIPUKO YA MABOMU

Miongo inayokuja baada ya kuangamia kwa binadamu itaathiriwa na umwagikaji wa mafuta , kuvuja kwa kemikali na milipuko ya viwango vya aina yake ya mabomu yote ambayo mwanadamu atakuwa ameyaacha.

Baadhi ya matukio hayo yanaweza kusababisha moto ambao unaweza kuwaka kwa miongo mingi. Chini ya mji wa Centralia katika jimbo la Pennsylvania, safu ya mkaa imekuwa ikiwaka tangu 1962, na hivyobasi kulazimu wenyeji wa eneo hilo kuondoka na mji huo kuharibiwa.

Hii leo eneo hilo linaonyesha barabara zilizotengenezwa mbali na moshi unaofuka. Uasilia au maumbile yamechukua sakafu ya eneo hilo. **BBC**



HABARI DODOMA

## Uzalishaji wa mkonge ulivyoongezeka nchini

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imesema uzalishaji wa zao la mkonge nchini umepanda kutoka tani 19,700 mwaka 1970, hadi kufikia tani 36,000 mwaka 2019.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema uzalishaji huo kwa sasa hauridhishi ikilinganishwa na fursa zilizopo kwenye sekta ya mkonge.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa inafikia uzalishaji wa tani 120,000 ifikapo mwaka 2025.

Mgumba, alisema kuwa lengo la serikali ni kujadili na kuzipatia majawabu changamoto katika zao la mkonge nchini, ili kuongeza tija katika uzalishaji, ajira na kukuza sekta ya viwanda, pato la mkulima na taifa kwa ujumla.

Alisema, pamoja na changamoto hizo, serikali inashughulikia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza tija na uzalishaji, kwa kuanzisha vitalu vya mbegu ya mkonge katika halmashauri zote ambako zao la mkonge linastawi.

Aidha, kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Mlingano, uzalishaji wa mbegu bora umeanza ili kuzalishwa kwa wingi.

Pia alisema serikali inafanya uhakiki wa mashamba ya mkonge yaliyobinafsishwa ili yaweze kuzalisha, kama ilivyokubaliwa kwenye mikataba, ikiwamo kutoa elimu kwa maofisa ugani katika vijiji na kata kwenye maeneo yanayolima zao hilo.

Alifafanua kuwa mambo mengine yanayofanywa na serikali ni kuongeza bajeti na kuwezesha kituo cha Utafiti Mlingano ili kufanya utafiti wa aina mbalimbali za mbegu ya mkonge na kuzisambaza kwa wakulima.

Hata hivyo, Naibu Waziri huyo, alisema kuhimiza na kushawishi wawekezaji kuwekeza mnyororo wa thamani wa tasnia ya mkonge hususani kwenye viwanda na teknolojia bora za uzalishaji wa bidhaa za zao hilo.

Alisema mikakati ambayo serikali imeanza kuitekeleza na mafanikio yake yanahitaji ushiriki wa pamoja wa wadau wote wa tasnia ya mkonge.

Vile vile, Mgumba alisisitiza kuweka utaratibu na kukubaliana namna bora ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, utoaji wa elimu kwa wakulima na maofisa ugani.

Hata hivyo, alisema kuwa umefika wakati sasa wakulima kulima kilimo cha kisasa na cha kibiashara ili kuongeza uzalishaji na kuhimili ushindani wa soko la dunia.

# Askofu afunda Watanzania kuingia uchumi wa kati

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

ASKOFU wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT) Kanda ya Kati, Julius Bundala, amewataka Watanzania kutobweteka na kuacha kufanya kazi kwa bidii, kutokana na Benki ya Dunia kuitangaza kuingia katika uchumi wa kati.

Askofu Bundala aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu Tanzania kuingia katika orodha ya nchi zenye uchumi wa kati.

Alisema Watanzania hawatakiwi kubweteka, kutokana na tangazo hilo bali wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania zaidi ya hapo ulipofikia.

"Tunashukuru kwa tangazo hili la Benki ya Dunia kwani mara nyingi tumekuwa tukisikia uchumi ukikua kwa asilimia sita, lakini hivi sasa tumepanda hadi katika kufikia kiwango cha uchumi wa kati," alisema Askofu Bundala.

Pia alisema kuwa kufikia kiwango hicho kilichotangazwa siyo sehemu ya kuwafanya Watanzania kuacha kujituma na kufanya kazi kwa bidii kama ilivyokuwa awali.

"Sisi hatujaandikiwa na Mungu kuwa ni wa uchumi wa kati bali kama tutaendeleza kujituma na chini ya viongozi wetu wakuu wa nchi katika awamu hii tutapanda kiuchumi hata kufikia katika ule uchumi wa juu kama mataifa mengine duniani," alifafanua.

Vile vile, alisema kuwa kama taifa ili kufikia uchumi wa juu linatakiwa kuweka mikakati ambayo itasaidia kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ili kusafirisha na kuuza nje.

Aidha, askofu huyo alisema wanamwomba Mungu katika uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu, kupatikana viongozi bora wenye hofu ya Mungu ambao watasaidia kukiendeleza kile kilichopatikana katika miaka mitano.

"Tunamuomba Mungu alete viongozi ambao wataweza kuendeleza kazi hii nzuri ili kuendeleza maendeleo haya pamoja na kuongeza kasi zaidi ya kuyafikia maendeleo ya juu," alisema Askofu Bundala.

Alitoa wito kwa Watanzania, kuhakikisha wakati wa kupiga kura wanachagua viongozi mbalimbali wanaoshiriki kikamilifu ili kumchagua kiongozi bora atayewaongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

"Kila muumini, kila Mtanzania, anatakiwa kushiriki katika zoezi hili la kupiga kura ili kumchagua kiongozi bora na siyo kuchaguliwa na watu viongozi watakao muongoza," alisema.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Koplo Athumani Rashidi, akitoa elimu kwenye warsha kwa ajili ya watu wenye ulemavu na viongozi wa vyama vya siasa jijini Dodoma jana, juu ya umuhimu wa kuyalinda makundi maalumu wakati wa mikutano ya kampeni ya uchaguzi wa vyama vya siasa, utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri aonya wasimamizi wa mirathi

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ameonya wasimamizi wa mirathi na mali za marehemu kuacha kutumia kwa manufaa yao binafsi huku familia zikitaabika.

Mhagama alitoa onyo hilo, mwishoni mwa wiki wakati akizungumza kwenye mkutano na vijana wanaoishi na Virusi (VVU) vya Ukimwi ambao wapo chini ya Baraza la Watu Waishio na VVU (NACOPHA) kwa ufadhili wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi nchini (TACAIDS).

Alisema kuwa wapo baadhi ya watu ambao si waaminifu na wamekuwa wakitumia mali au mirathi ya marehemu kwa ajili ya kujinufaisha badala ya kutumia kwa lengo lililokusudiwa.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikisababisha watoto wa marehemu kukosa haki yao ya msingi ya kunufaika na mali ikiwa ni pamoja na kushindwa kupelekwa shule kwa kukosa mahitaji muhimu.

"Hili ni tatizo kubwa sana ambalo tunatakiwa kulipiga vita, wadau pamoja na serikali tunatakiwa kusimamia suala hili kwa kuwalinda watoto hawa kupata stahiki zao baada ya wazazi wao kufariki," alisema Mhagama.

Aliongeza: "Tunaona asilimia kubwa ya watoto hawa wanakosa haki yao ya msingi ya kupata elimu, sababu kubwa ni wasimamizi wa mirathi au ndugu ambao si waaminifu, hatutawafumbia macho watu wa aina hiyo."

Hata hivyo, aliwataka vijana hao kupitia vikundi vyao wawe wanachangamkia fursa ambazo zinapatikana ikiwa ni pamoja na kupata mikopo ya vijana ambayo itawasaidia kukuza uchumi wao.

Alisema serikali itakuwa pamoja nao, katika kila hatua ikiwamo kuwawezesha ili nao watoe mchango katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana hao, Pudensiana Mbwiliza, alisema wanamwomba Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuwa mlezi wao.

Alisema wanatambua heshima na mafanikio aliyonayo kitaifa kama vile kuwa balozi wa kampeni ya furaha yangu inayohamasisha wanaume kupima VVU.

Hata hivyo, alisema wako katika wakati mgumu baada ya wazazi wao kufariki, kwani wamepoteza vitu vya thamani ambavyo vimechukuliwa na ndugu na watu waliochaguliwa kusimamia mirathi na mali za familia zao.

Alivitaja baadhi ya vitu hivyo kuwa ni nyumba, mashamba, ardhi na biashara hali inayowafanya baadhi ya watoto kuangukia kwenye umaskini na kuwa tegemezi pamoja na kukosa msaada.

Alisema kutokana na hayo baadhi ya watoto wa kike wamekuwa wakijiingiza kwenye biashara ya ngono na matumizi ya dawa za kulevya jambo ambalo ni hatari kwani inaweza kuchangia kuongeza maambukizi mapya ya VVU.





# TAKUKURU yavitaka vyama kupinga rushwa

**Na Innocent Ng'oko, MBARALI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Mbarali, imevitaka vyama vyote vya siasa kushirikiana na taasisi hiyo kukabiliana na vitendo vya rushwa katika mchakato wa kuwapata wagombea wa udiwani na ubunge wenye sifa ndani ya vyama vyao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa TAKUKURU wilayani Mbarali, Nicolas Mwambene, wakati akizungumza na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kata ya Igurusi kuhusu umuhimu wa kuelewa na kuzingatia sheria ya gharama ya uchaguzi na kubainisha kuwa muda wa viongozi wanaopatikana kwa vitendo vya rushwa umekwisha.

Mwambene alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wagombea kuwarubuni viongozi na wanachama ndani ya vyama vyao kwa kuwapa zawadi mbalimbali zikiwamo fedha kwa lengo la kujipatia madaraka.

Alisema katika mchakato wa kuwapata wagombea mbalimbali wa udiwani na ubunge, CCM imekuwa mstari wa mbele katika wilaya hiyo kuwaalika katika vikao vyao vya ngazi ya kata na wilaya kwa lengo la kutoa elimu ya sheria ya gharama za uchaguzi.

Aliviomba vyama vingine vya siasa kutoa mialiko katika ofisi yake ili waweze kupatiwa elimu ya kukabiliana na vitendo vya rushwa katika uchaguzi wa mwaka huu ndani ya vyama ili waweze kupata viongozi bora.

Alisema TAKUKURU imejipanga kukomesha vitendo vya rushwa katika mchakato wa kuwapata wagombea ndani ya vyama vya siasa ili kupata viongozi bora katika uchaguzi wa mwaka huu.

Kwa upande wake, Katibu wa CCM Kata ya Igurusi, Pendo Mwakaponda, alisema CCM Igurusi imejipanga kushirikiana na TAKUKURU kwa lengo la kukabiliana na wagombea ndani ya chama ambao wamejipanga kutoa rushwa kwa wapiga kura ili waweze kupitishwa.

Mwakaponda alisema mgombea urais wa CCM, John Magufuli, anaichukia rushwa waziwazi na kuwa chama kimejipanga kumchagulia viongozi wenye sifa ambao watamsaidia kwa dhati katika serikali yake ili kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema kwa miaka mitano, chama hicho chini ya Diwani wa CCM kimefanikiwa kufanya shughuli za maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwamo ujenzi wa barabara, shule na usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali ya kata.

# Wauguzi walalamikia mgawo CHF

**Nebart Msokwa, BUSOKELO**

WAUGUZI katika Hospitali Teule ya Itete katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wamesema mfumo mpya wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa unawachonganisha wauguzi na wagonjwa wakati wa utoaji huduma za afya.

Wakizungumza mbele ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Jimbo la Busokelo ambayo imetembelea hospitali hiyo kukagua mradi wa upanuzi wa hospitali hiyo, baadhi ya wauguzi walisema kuwa CHF inayodaiwa kuwa imeboreshwa haina uhalisia kutokana na mgawo wa fedha unaopelekwa kwenye hospitali na huduma wanazopaswa kupewa wagonjwa wenye kadi za bima hiyo.

Muuguzi Mkuu wa hospitali hiyo, Tumwitikege Mwambona, alisema Halmashauri ya Busokelo inapokusanya fedha za CHF huzigawa kwa kuzingatia hadhi ya hospitali bila kujali gharama za matibabu zilizotolewa kwa wagonjwa wenye kadi za CHF wanaokwenda kutibiwa.

Alisema, pia kwenye hospitali zenye hadhi sawa hupewa kiwango sawa cha fedha za CHF bila kujali idadi ya wagonjwa waliotibiwa, aina ya maradhi, wala gharama ambazo hospitali imetumia.

"Kwa mfano fedha za CHF zikipatikana milioni tano zinagawiwa kwanza kwa kufuata hadhi ya hospitali ambapo hospitali za rufani zinapata zaidi na hospitali za halmashauri zinafuata, lakini kibaya zaidi hospitali zenye hadhi ya halmashauri zinagawiwa kiwango cha fedha kinacholingana, hali hii inasababisha mwisho wa mwezi hospitali inapewa shilingi laki moja wakati sisi tumetumia zaidi ya milioni mbili," alisema Tumwitikege.

Alisema hali hiyo inasababisha hospitali kushindwa kununua dawa kwa ajili ya wagonjwa wenye kadi ya CHF, na hivyo baada ya kuwafanyia vipimo na kujua maradhi yao huwaeleza wakanunue dawa wenyewe.

Kadhalika, alisema hali hiyo husababisha huduma kwa wagonjwa wa CHF kutofautiana na wagonjwa wenye kadi za Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), ambao hutibiwa bila shida.

Tumwitikege alisema wagonjwa wa CHF wanapoona huduma wanayopewa inatofautiana na wanayopewa wagonjwa wa NHIF, huwalalamikia wauguzi kuwa wanapendelea bila kujua kuwa sio kwa matakwa ya wauguzi.

"Mgonjwa hajui changamoto tulizonazo, anachohitaji ni huduma kwa vile wanaofanya maamuzi haya huwa hawapo au hawakutani na wagonjwa ana kwa ana, lawama zote tunazibeba sisi, yaani kwa kifupi naweza kusema CHF haijaboreshwa bali inatufanya wauguzi tulaumiwe zaidi," alisema Tumwitikege.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, alisema suala hilo ni la kisera na yeye hana uwezo wa kulishughulikia kwa vile maamuzi ya namna ya kushughulikia suala la CHF yanatoka wizarani.

"Ninachoweza kusema ni kwamba suala hili liko nje ya uwezo wangu, hii ni kwasababu maamuzi yote kuhusu CHF yanatoka wizarani na sisi ni watekelezaji tu," alisema Ngilangwa.

Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, alisema suala hilo amelichukua na atalifikishwa kwa wahusika ili lifanyiwe kazi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Galijembe, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakati Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mkoa huo, ilipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa shule hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RPC ahimiza ushirikiano kutokomeza uhalifu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KAMANDA wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, amewataka wananchi wa Wilaya ya Chunya kushirikiana na Jeshi la Polisi kutokomeza uhalifu unaofanyika kwenye jamii.

Aliyasema hayo juzi wakati alipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya Jeshi la Polisi na kuwataka wananchi kutoa taarifa za wahalifu ili kuliwezesha jeshi hilo kuwadhibiti kabla hawajatekeleza uhalifu wao.

Alishauri pia vikundi vya kijamii vya ulinzi shirikishi (Sungusungu), kusaidia kudhibiti wahalifu hasa wezi nyakati za usiku kwa kuwakagua watu wote wanaotembea usiku na kila anayekutwa na silaha aitolee maelezo.

Vilevile, aliwataka wananchi kuepuka kudhurura usiku na kuacha nyumba zao bila ulinzi kwa maelezo kuwa wezi huwa wanautumia mwanya huo kuingia na kuiba mali zao.

"Ninyi watu wa Sungusungu wakagueni watu ambao wanatembea usiku, kuna mwingine unapishana naye amevaa koti kumbe humo ndani ana 'kisilaha' chake, sasa ni lazima tufanye kazi kwa ushirikiano ili kutokomeza wahalifu wa aina hii," alisema Kamanda Matei.


Aliwaomba viongozi wa vijiji na kata kusimamia taratibu za uendeshaji wa kumbi za starehe kwa kuhakikisha wamiliki hawaziendeshi mpaka muda ulioruhusiwa kwa kuwa unachochea vitendo vya uhalifu.Alisema baadhi ya baa zinafanya kazi usiku kucha kitu ambacho ni kinyume na utaratibu na kusisitiza maeneo kama hayo kuzuiliwa kuendelea na shughuli hizo.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei, aliwaomba viongozi wa kata kuyafufua mabaraza ya kata ya ardhi ili yasaidie kusuluhisha baadhi ya kesi ndogo badala ya kila kesi kupelekwa kwenye vituo vya polisi na kusababisha msongamano wa mahabusu.

Alisema ili kuhakikisha vijiji na kata vinakuwa salama, viongozi wa maeneo hayo wanatakiwa kuhuisha mara kwa mara daftari la wakazi wa maeneo yao ili kuwadhibiti wageni ambao wanaingia kinyemela na kuanza kutekeleza uhalifu.

"Lakini mkumbuke kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, hivyo nawaomba viongozi mwendelee kuwaelimisha wananchi ili washiriki zoezi hilo kwa amani na kuhakikisha wanawachagua viongozi bora," alisema Matei.

Pia aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuwalea watoto katika malezi bora ili kuwaepusha na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ikiwamo kubakwa na kufanyiwa vitendo vingine vya kikatili hasa kwenye maeneo ya migodini na mashambani.





# Wanawake wajikwamua, wajiwekea mil. 116/-

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANAWAKE wanaoishi katika hali ya umaskini Unguja na Pemba hatimaye wamejikwamua kiuchumi baada ya kuingia kwenye vikundi vya kuweka na kukopa (VSL), kwa pamoja wameweka jumla ya Sh. 116,560,750 kuanzia mwezi wa Juni, mwaka jana hadi sasa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema wanawake ambao wameingia katika mpango wa kuwawezesha kuiuchumi Zanzibar unaojulikana kwa jina la WEZA, umewafikia wanawake wapatao 1,207 kati yao 513 ni kutoka Unguja na 694 kutoka Pemba.

Alisema wanawake hao kutoka katika shehia 21, walijiwekea kiasi hicho cha fedha baada ya kuweka kila wiki kiasi cha wastani wa Sh. 500 kila mtu hadi 10,000 na pia kujiingiza katika utengenezaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo sabuni za aina tofauti za viungo kama karafuu, liwa na manjano.

Pia wanafanyakazi ya ufumaji wa nguo na mashuka pamoja na ufugaji.

"Wanawake walijiunga na vikundi vya kuweka na kukopa maarufu kwa jina la WEZA vimeleta mabadiliko makubwa kwa vijana na kubadili mfumo wa maisha yao na kuweza kuendesha familia zao vizuri," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Maisha Siri, Hadia Hashim Awesu, kutoka Mkanyageni Pemba, alisema kuwapo kwa vikundi hivyo kwa kiasi kikubwa kumesaidia kuwainua wanawake.

"Mpaka sasa tumeweka jumla ya Sh. 3,584,000 kupitia uwekaji wa hisa, mtu mmoja huweka kati ya 2,000 hadi 10,000 kwa wiki," alisema.

Fatuma Mohamed Juma, mwanachama wa kikundi hicho alisema licha ya maendeleo ya pamoja kwa kikundi hicho, pia kimesaidia kuinua kiuchumi kwa mwanachama mmoja mmoja kupitia uchukuaji wa mikopo kwenye mfuko wa hisa.

"Nilipojiunga katika kikundi nilikopa Sh. 300,000 kwa ajili ya kununua cherehani nyingine ya kisasa kwa kuwa wateja wameongezeka... nashukuru nimepata mafanikio makubwa," alisema.

Mradi wa WEZA unatekelezwa na TAMWA kwa kushirikiana na Milele Foundation (ZMF), ukiwa umejikita kuwawezesha wanawake na vijana kiuchumi.

# Maaskofu wapya Zanzibar waaswa kuacha ubinafsi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ASKOFU wa makanisa ya PEFA Tanzania Elirehema Logilunore Mollel, amewataka maaskofu wapya waliosimikwa kutumikia nafasi hiyo kuacha ubinafsi badala yake watumikia jamii na kuepuka kugombania madaraka.

Mollel aliyasema hayo katika hafla ya kuwasimika maaskofu wapya watano katika Kanisa la PEFA Kisauni, Wilaya ya Magharibi B, Unguja.

Alisema kuwa kazi ya mtumishi wa umma ni kutumikia jamii kwa imani thabiti na sio kutaka kitu kutoka kwao na kuwakandamiza.

"Utumishi umebadilika na kuwa utumishi wa kutafuta mamlaka na kuonea watu," alisema Mollel.

Alisema tofauti zao katika ukubwa wao isiwe sababu za kutaka kuwakandamiza walio chini bali wamekuja kuwatumikia watu na kuwasaidia shida zao. "Kazi yetu sisi ni kutumika, hatuhitaji kuwa na watu watakaoleta utengano, migogoro ndani ya nyumba za Mungu na wala usitafute mbinu ya kuanza kumrubuni mkuu wako kwa kutaka madaraka," alisema.

Naye Askofu wa makanisa ya PEFA Zanzibar, Dk. Daniel Kwilemba Kwiyeya, aliwataka maaskofu hao kuendeleza ushirikiano ndani ya makanisa yao kwa lengo la kuweka usawa na umoja miongoni mwao.

Alisema kuwa nafasi ambayo wameipata wanaweza kushinda kama watatii neno la Mungu na kuhimiza ushirikiano baina yao.

Jumla ya maaskofu wapya watano walisimikwa katika kanisa hilo ambao watapewa kazi ya kuwahubiri waumini wa dini hiyo na kutakiwa kuacha ubinafsi na kutumikia jamii ili kupata neema kutoka kwa Mungu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na familia ya marehemu Haji Nassib Haji (Nyanya), alipofika nyumbani kwa marehemu Bububu kwa Nyanya, Zanzibar kutoa mkono wa pole. Kulia ni mkewe, Mama Mwanamwema Shein na mjane wa marehemu Zainab Nyanya. PICHA: IKULU

# Wahitimu kidato cha sita watakiwa kujiendeleza

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANAFUNZI waliomaliza kidato cha sita wa Shule ya Sekondari Hamamni, wametakiwa kutoridhika na elimu waliyoipata, wajiendeleze zaidi ili nchi ipate wasomi.

Akizungumza katika mahafali ya tano ya kidato cha sita katika shule hiyo mjini Unguja, Mkurugenzi Idara ya Utumishi na Uendeshaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Omar Ali Omar, alisema taifa bado linahitaji wataalamu wa fani mbalimbali hivyo ipo haja kwa wahitimu hao kuzidisha bidii katika masomo ili kufikia malengo hayo.

Alisema kutafuta elimu ni jambo muhimu katika maisha ya mwanadamu na ndio maana likatiliwa mkazo mpaka katika vitabu vyote vya dini.

Aliwapongeza walimu wa shule hiyo kwa kujitolea mpaka muda wa ziada wa kazi kuhakikisha wanafunzi wao wanafanya vizuri katika mitihani yao.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ali Rashid, aliwataka wahitimu hao kuwa mabalozi wazuri wanapokuwa mitaani na kutambua kuwa bado wanasafari ndefu ya kutafuta elimu.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wenzake, mwanafunzi Dalila Mohamed, alisema pamoja na kuwa Wizara ya Elimu imeimarisha mambo mengi katika elimu, bado wana tatizo la ukosefu wa majisafi na salama katika shule yao na kuiomba wizara hiyo kulipatia ufumbuzi suala hilo.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ina ghorofa moja, ina godown ina fremu 10 na ina eneo kubwa wazi, ipo Dar es Salaam. Mawasiliano 0757 079057


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA CHETI



**Mashukura Habibu** anatangaza kupotea kwa cheti cha Ualimu chenye **index namba E0504-0064** kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Katoke Mkoa wa Kagera mwaka 2010. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KAG/MUL/RB/293670/2020**

115809102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo . PONGWE TANGA.....**
**Usimamizi wa Mirathi....................2020.........................**

**Ombi la CHADA ABDALLAH RAMADANI ...kuteuliwa Msimamizi mirathi ya marehemu MWANAKUZI MBARAJI**

**Kwa..........................**
**YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa nauhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 14/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kutenguliwa Tarehe 3/7/2020

MAHAKAMA YA MWANZO

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

215809702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 2020**

**Ombi la SECHE YONA NGHAKAMO kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu LEAH YONA NGHAKAMO**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 2/7/2020

PRINCIPAL
PRIMARY COURT
URBAN DODOMA

115808102

**MAHAKAMA YA TANZANIA (JUDICIARY)**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU**
**MKAZI MOROGORO**

**SHAURI LA TALAKA NA. 1/2020**

**MWOMBAJI........NEEMA JOSEPH MNYENYELWA**
**DHIDI YA**
**MJIBU MAOMBI........EMMANUEL BONZA BARIDI**

**KWA: EMMANUEL BONZA BARIDI**

POPOTE ULIPO.
Mahakama hii inakufahamisha kwamba Mwombaji amefungua madai ya talaka dhidi yako,nakala ya madai hayo inapatikana katika Mahakama hii.

Shauri hili lilisikilizwa upande mmoja na limepangwa kusomwa hukumu mnamo tarehe 22/07/2020 saa 2:30 asubuhi.Kwa wito huu,Unatakiwa kuwepo Mahakamani Siku husika.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 6 mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI
MOROGORO

115809802

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IDDY HASSAN NDEE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **T- BETTER** yenye namba za usajili **MC 587 CFZ.** Chassis no.**LZEPCLOXK4109186,** Engine no.ZJI62FMJK4109186.Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi **DOD/KON/RB/324457/2020.**

115810702

## KUPOTEA KWA KADI

**Frida M. Mosha** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SPACIO,yenye namba ya usajili **T917 DEC** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Chasis namba **NZE121343772,** Engine namba **TA-NZE121N.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**KAW/RB/2020**

115809002


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Mwandishi wa habari anusurika kwenda jela, alipa faini ya mil. 5/-

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MWANDISHI wa Habari, Albert Sengo, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 5 au kwenda jela miezi 12, kwa kosa la kuchapisha maudhui mtandaoni kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Gwae Sumaye, na mwandishi huyo alikwepa adhabu ya kwenda jela kwa kulipa faini na kuwa huru.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu huyo alisema mwandishi huyo alivunja kifungu cha 18 cha kanuni za maudhui ya mtandaoni, na kwamba adhabu zake ni faini , kwenda jela au vyote kwa pamoja.

Kesi hiyo yenye namba 101 ya mwaka 2020 ilisomwa kwa mara ya kwanza April 23, kwa madai ya mtuhuhumiwa huyo kuendesha televisheni mtandaoni (online TV) bila usajili, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni za maudhui za kimtandao za mwaka 2018.

Sengo alikamatwa Machi 23, mwaka huu na maofisa wa upelelezi wa Jeshi la Polisi, toka kitengo cha uhalifu wa mtandaoni mkoani Mwanza na baadaye aliachiwa kwa dhamana hadi April 24 alipokamatwa tena na kufunguliwa mashtaka kisha kuachiwa kwa dhamana.

Mwenyekiti wa Chama Cha Waandishi wa Habari mkoani Mwanza, Edwinn Soko, alisema waliratibu upatikanaji wa fedha za kulipa faini na kufanikiwa kumnusuru mwanatasnia mwenzao asiende gerezani.

## Wapewa mchongo kukuza biashara

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

WAJASIRIAMALI wadogo wamekumbushwa kutoridhika na nafasi walizo nazo badala yake wawe wabunifu wa bidhaa wanazotengeneza na kuwa na ndoto za kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Wito huo ulitolewa juzi na Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Wilaya ya Mkuranga, Safina Msemo, wakati wa mafunzo ya siku moja kwa kundi la wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao wanapatiwa mikopo katika wilaya hiyo.

Safina alisema ubora wa bidhaa ndio utakaowezesha wajasiriamali kuwa na mabadiliko na kukua kiuchumi kwa bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

"Tuwe na mfumo mzuri wa utafutaji wa masoko, tuhakikishe bidhaa zinahifadhiwa katika mazingira safi na kutoridhika na biashara tulizonazo tujiwekee malengo ya kuwa wafanyabiashara wakubwa," alisema Yussuph.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkuranga, Veronica Kinyemi, aliwasisitiza wajasiriamali kitumia fursa zilizopo kufanya shughuli za uzalishaji na kukuza bidhaa zao.

"Wilaya yetu ipo jirani na Jiji la Dar es Saalam, hivyo tutumie fursa ya masoko yaliyopo kupeleka bidhaa zetu huko na kwa watendaji wote mliopo hapa simamieni vizuri vikundi vilivyopo kwenye maeneo yenu viende kwenye malengo yaliyokusudiwa na kuleta matokeo tarajiwa," alisisitiza.

Akiongea kwa niaba ya Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Mratibu wa Dawati la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Sylvia Tumaini, alisema mafunzo hayo yalilenga vikundi 11 ambavyo vitapatiwa mikopo ya Sh. milioni 61.

Tumaini alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20, zaidi ya Sh. milioni 553 sawa na asilimia 110.64 zilitolewa kwa vikundi 110 vikiwamo 35 vya vijana, vinne vya walemavu na wanawake 71.




Mkurugenzi wa Uendeshaji Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mbaruku Magawa (wa pili kulia), akitoa ufafanuzi masuala ya mfuko huo kwa wananchi waliofika katika banda la PSSSF, katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyomalizika jana. Kulia ni Ofisa Uhusiano Mkuu wa Mfuko huo, Abdul Njaidi na aliyekaa wa pili kushoto ni Ofisa Matekelezo Mwandamizi wa Mfuko, Donald Meeda. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wagombea waonywa kuhusu rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAGOMBEA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wameonywa kuhusu kujihusisha na vitendo vya rushwa huku wakikumbushwa kuzingatia miongozo ya kugombea pamoja na maadili.

Katibu wa CHADEMA Jimbo la Kibaha Mjini, Michael Nkobi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kufunga uchukuaji na urejeshaji fomu za kugombea nafasi ya ubunge katika jimbo hilo.

Nkobi alisema chama hakitasita kuwachukulia hatua kwa watakaobainika kijihusisha na rushwa na kukiuka kanuni na taratibu za kampeni.

"Hatutasita kuchukua hatua kwa taarifa za rushwa na atakayebainika kukiuka kanuni na miongozo ya chama chetu na kanuni za kampeni zitakapokiukwa," alisema Nkobi.

Akirudisha fomu ya kuomba kuchaguliwa kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, Michael Mtally alisema amelazimika kwa mara nyingine kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kutokana na hali ya maendeleo kutoendana na kasi ya Rais John Magufuli.

Mtally alisema endapo atapitishwa na chama chake na hatimaye kuchaguliwa, ana mipango ya kuwashirikisha wananchi katika kuibua miradi ya maendeleo ambayo itakuwa mkombozi kwao.

"Nitajikita zaidi kuongeza vyumba vya madarasa, ujenzi wa zahanati na kuboresha huduma za afya hususani kwa wazee ambao wanatakiwa kutibiwa bure pamoja na kuhakikisha dawa zinapatikana kwa urahisi kuondoa usumbufu kwa kundi hilo," alisema Mtally.

Naye Mery Muro ambaye amemaliza muda wake wa ubunge wa Viti Maalum kupitia chama hicho, alisema kwa kipindi cha miaka mitano ameyafahamu vizuri mahitaji ya wananchi, hivyo amechukua fomu ya kuomba kuchaguliwa kugombea Jimbo la Kibaha Mjini na Viti Maalumu kushughulikia matatizo hayo.

Mwenyekiti wa Jimbo la Kibaha Mjini, Moses Mgae, alisema chama hicho kimejipanga kuchukua nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa kitapitisha wagombea wenye uwezo na wanaokidhi kuongoza wananchi.

Muro na Mtally walichukua fomu za nafasi ya ubunge Kibaha Mjini, huku viti maalumu wakichukua Rehema Yusuph, Konjo Sinze.

## 'Vyama visitumie wanawake mawakala wa kuvunja amani'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VYAMA vya siasa nchini vimetakiwa kutowatumia wanawake kama mawakala wa kuvunja amani na utulivu wa nchi katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2020.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira,Vijana na watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama, alipokuwa akizungumza na wanawake viongozi wa vyama hivyo katika kikao cha kumpongeza kwa utendaji wake.

Alisema vyama hivyo visiwatumie wanawake kwa faida zao na kuwafanya mawakala wa vurugu nchini, bali wawaache wapambane kutafuta haki yao kwa misingi ya sheria na taratibu kwa kuwapa fursa na wao kugombea.

"Kama amani ikivunjika muathirika wa kwanza ni mwanamke, wa pili ni mtoto, niwaombe sana wanawake sisi tuwe mawakala wa amani ili uchaguzi upite salama, lakini wasitumike kuvunja amani na utulivu wa Taifa letu, mwanamke asili yake ni wakala wa amani," alisema.

Mhagama alivisisitiza vyama hivyo kuwaacha wanawake kushiriki kwenye uchaguzi ili washinde na wapate fursa ya kuwa viongozi wa ngazi mbalimbali.

# MOURINHO AIDHARAU LIGI YA EUROPA



**LONDON,** England

JOSE Mourinho anataka kuiongoza Tottenham kwenye Ligi ya Europa, lakini amelinganisha kucheza kwenye mashindano hayo sawa na Lewis Hamilton kushinda Formula Two.

Spurs ilishinda 2-1 kwenye Ligi Kuu dhidi ya Arsenal katika 'dabi' ya London Kaskazini Jumapili, wakajiweka nafasi ya nane kwenye msimamo na kuongeza nafasi ya kufuzu kwenye mashindano hayo ya Ulaya.

Mourinho yupo tayari kufuzu kwenye Ligi ya Europa, ingawa kocha huyo wa Spurs amelinganisha michuano hiyo sawa na mshindi wa mbio za magari za Formula One, Hamilton kwenda kushindana kwenye daraja la chini.

"Ligi ya Europa sio mashindano makubwa Ulaya," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini ni ya pili na wakati klabu inashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya au mchezaji anashinda ni sawa, lakini kucheza kwenye Ligi ya Europa ni sawa na Hamilton kushinda mbio za magari za daraja la chini kitu ambacho sio cha kujivunia.

"Lakini ni mashindano na naona sawa kucheza kwenye Ligi ya Europa kuliko kushindwa kufuzu.

"Nafikiri ni taji ambalo Tottenham wangependa kulishinda. Bila shaka Manchester United, ni klabu yenye malengo makubwa na inafikiria zaidi kuhusu Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini tulicheza kwenye Ligi ya Europa na tulishinda."

# Klopp awapa tano makinda

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amewaambia wachezaji wake vijana wa Liverpool wanaweza kuwa "wazuri" kwa siku za usoni kama wataendelea kuimarika.

Wachezaji kama Curtis Jones mwenye umri wa miaka 19, na Neco Williams mwenye miaka 19, wanapewa nafasi ya kucheza mechi za hivi karibuni kwa mabingwa hao, ambao walilazimishwa sare ya bao 1-1 na Burnley Jumamosi, huku Harvey Elliott mwenye umri wa miaka 17, alicheza mechi mbili za Ligi Kuu msimu huu.

Liverpool inahitaji ushindi katika mechi zake tatu zilizobaki ili kuvunja rekodi ya Manchester City ya kufikisha pointi 100 kwa msimu mmoja wa Ligi Kuu ya England.

Klopp, ambaye timu yake itacheza na Arsenal Jumatano, alisema vijana hao wana nafasi kubwa ya kukua.

"Sina uhakika, lakini inategemea na vijana wenyewe wapo tayari kwa namna gani?" Alisema akinukuliwa na vyombo vya habari vya Uingereza.

"Hakuna mchezaji mzee na kijana, wote wazuri na nina matumaini watakuwa bora zaidi kwa siku za usoni."





# Kocha PSG aihofia Atalanta

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel anatarajia ushindani mkubwa kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta, lakini akili yake inaangalia sehemu nyingine.

Mashabiki 5,000 walihudhuria wakati PSG ilipoifumua Le Havre mabao 9-0 kwenye mchezo wa kirafiki Jumapili.

PSG imepangwa kuikabili Atalanta kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali, lakini wanakabiliwa na fainali ya Kombe la Coupe de France dhidi ya Saint-Etienne na Kombe la Coupe de la Ligue dhidi ya Lyon.

Tuchel alisema anajua PSG watakuwa na mtihani dhidi ya Atalanta mjini Lisbon Agosti, lakini sasa akili yake inaangalia kwanza mataji ya nyumbani.

"Utakuwa mchezo mgumu, lakini haishangazi kwa sababu tutacheza robo fainali. Kuna timu nane zinazotaka kushinda mashindano. Kila timu inaweza kushinda mechi zake tatu," alisema kocha huyo.

"Naamini utakuwa mchezo mgumu dhidi ya Atalanta, utakuwa mgumu sana. Wana wachezaji wenye ubora. Tumeona hilo wakati walipokuwa wanacheza dhidi ya Juventus (Jumamosi). Ni timu yenye uwiano mzuri na wanajua kujilinda. Lakini sasa hatuwezi kufikiria kuhusu hilo."

## HABARI MICHEZO

# Messi atasaini mkataba mpya Barcelona - Bartomeu

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amesisitiza nyota wao, Lionel Messi atasaini mkataba mpya na miamba hao wa LaLiga.

Messi mwenye umri wa miaka 33, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka huku uvumi ukidai kuwa nahodha huyo ataondoka hapo Camp Nou mara tu mkataba wake utakapomalizika mwaka 2021.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, aliripotiwa kusitisha mazungumzo ya mkataba mpya na Barca ambao wanakimbizana na wapinzani wao Real Madrid kuwania ubingwa wa LaLiga msimu huu. Lakini Bartomeu anajiamini mfungaji huyo anayeongoza kwenye LaLiga, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo aliyoanza kuichezea mwaka 2004.

"Tumezungumza, tunazungumza na tutazungumza na Messi," alisema Bartomeu akiiambia TV3.

"Anataka kumaliza kipindi chake cha uchezaji hapa. Tutamwongezea mkataba mpya kwa uhakika kabisa, sina shaka ataendelea kuwa hapa."

Messi alitengeneza bao la ushindi kwa Arturo Vidal katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Real Valladolid.

Ilikuwa ni 'asisti' ya 20 kwenye LaLiga msimu huu na amekuwa mchezaji wa kwanza katika ligi kubwa tano Ulaya tangu Thierry Henry, kufunga na kutengeneza mabao 20 kwa msimu mmoja. Henry aliweka rekodi hiyo msimu wa 2002-03.

Ushindi huo uliwapa matumaini Barca kuendelea kuwa kwenye mbio za kuwania ubingwa wa LaLiga wakiwa na kocha wao Quique Setien. Setien alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo kutoka kwa Ernesto Valverde Januari, lakini kocha huyo wa zamani wa Real Betis amekuwa kwenye wakati mgumu kuonyesha kiwango chake na sasa wamepitwa pointi moja na Madrid ambao jana Jumatatu walikuwa wanacheza na Getafe.

Barca pia inajiandaa na mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-Bora dhidi ya Napoli baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. Mchezo wa kwanza walitoka sare ya kufungana bao 1-1.

Alipoulizwa kuhusu Setien, Bartomeu alisema: "Quique Setien atakuwa na timu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mpango ni kuwa na yeye kwa msimu ujao, malengo yetu ni kukamilisha mikataba."




# MBAPPE HAUZWI MSIMU HUU - PSG




**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain haitamuuza Kylian Mbappe kuelekea msimu wa 2020-21, lakini majaliwa ya Neymar bado hayajulikani, kwa mujibu wa L'Equipe.

Real Madrid haijaficha mpango wake wa kumwania Mbappe, huku Barcelona ikijaribu kutaka kumsajili tena Neymar.

Wakati PSG wakijiandaa na msimu wa 2020-21, mabingwa hao wa Ligue 1 wamefanya baadhi ya maamuzi ya usajili.

Mbappe amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kule Real Madrid kwa siku za usoni, hata hivyo mabingwa hao wa Ligue 1, PSG hawana mpango wa kumuuza nyota huyo wa Ufaransa kabla ya msimu ujao.

Lakini Neymar ameendelea kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na Barcelona baada ya kuondoka kule kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia mwaka 2017 na anaweza kuondoka wakati PSG wakiepuka kumwachia nyota huyo wa Brazil huru kwenye usajili wa mwaka 2022.

# *Solskjaer: Sina mpango kumwacha De Gea*

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer kamwe hajawahi kufikiria kumuacha David de Gea wakati kocha huyo wa Manchester United akiunga mkono kipa huyo wa muda mrefu kucheza tena kwa muongo mwingine na "kubeba mataji makubwa" hapo Old Trafford.

De Gea alizima rekodi ya Peter Schmeichel kuwa mchezaji kutoka nje aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa United, akifikisha mechi 399 wakati wakiibuka na ushindi wa 3-0 kwenye Ligi Kuu dhidi ya Aston Villa, Alhamisi iliyopita.

Licha ya kufikia mafanikio hayo, majaliwa ya De Gea yamekuwa mjadala mkubwa kutokana na makosa mengi anayoyafanya na sasa anapewa nafasi Dean Henderson ambaye yupo kwenye kiwango bora kule Sheffield United anakocheza kwa mkopo.

Lakini kocha wa United, Solskjaer alimsifia zaidi De Gea, ambaye ameshinda Kombe la Ligi Kuu, Ligi ya Europa, FA na EFL tangu atue hapo akitokea Atletico Madrid mwaka 2011.


"Haijawahi kunijia kwenye akili yangu hata mara moja," alisema Solskjaer wakati alipoulizwa kuhusu kumuacha De Gea kuelekea mchezo wa jana Jumatatu dhidi ya Southampton.

"Hapana kwa kweli. Kuwa golikipa wa Man Utd unatakiwa uwe imara. David yupo imara na anaweza kuwa hapa kwa muda mrefu zaidi."

Solskjaer, ambaye anaiongoza United ambayo haijashinda taji la Ligi Kuu ya England tangu mara ya mwisho ilipokuwa chini ya Alex Ferguson msimu wa 2012-13, aliongeza: "David amekuwa mchezaji bora tangu nimekuwa hapa na nimefurahi kufanya naye kazi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: KIPIGO SPURS NI MAJANGA ARSENAL

●●● Amsifu Mourinho, nafasi ya kushiriki michuano ya Ulaya sasa kutegemea...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anatambua kwamba kichapo cha Arsenal cha 2-1 kutoka kwa Tottenham ni "pigo kubwa" lakini alimsifia Jose Mourinho kwa kuwafanya kuwa kwenye maisha magumu.

Arsenal ilianza kuongoza katika dakika ya 16 kupitia kwa jitihada binafsi za Alexandre Lacazette katika mchezo huo wa 'dabi' ya London pale kwenye dimba la Tottenham Hotspur, lakini Son Heung-min aliiwahi pasi ya Sead Kolasinac kwenda kwa David Luiz na kusawazisha dakika tatu baadaye.

**Washikabunduki hao walikuwa kwenye kiwango cha kuvutia katika kipindi cha pili, lakini walijikuta kwenye wakati mgumu kuipita ngome ya Spurs, huku Toby Alderweireld akifunga bao la ushindi wa kikosi hicho cha Mourinho dakika tisa kabla ya mchezo kumalizika.**

Arsenal kwa sasa wapo nafasi ya tisa, huku mechi tatu zikiwa zimesalia, pointi nne nyuma ya Sheffield United waliopo nafasi ya saba, kufuzu kucheza mashindano ya Ulaya ingawa wanaweza kupata nafasi kama Manchester City adhabu yake ya kufungiwa miaka miwili kucheza mashindano ya Ulaya itathibitishwa.

"Kwa suala la pointi, ni pigo kubwa kwa sababu tulijua matokeo ya wikendi hii, lakini tutajaribu kuendelea kucheza kwa matumaini," alisema Arteta.

"Tutapambana kwenye ligi na Kombe la FA kucheza kwa ubora wetu na kujaribu kumaliza tukiwa imara kadri inavyowezekana."

Aliongeza: "Nimekatishwa tamaa na kuhudhunika. Kwa sababu kipindi cha kwanza tulicheza vizuri na kuonyesha kiwango chetu, lakini baadaye wakatushinda."

## ZISIKUPITE

### INTER YAMTAKA KANTE

INTER Milan inafikiria kumsajili kiungo wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, huku Blues hao wakiwa tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Gazzetta dello Sport, via Metro)***

### JOVIV AWINDWA AC MILAN

AC Milan inamwania straika wa Real Madrid na Serbia, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 22, ambaye anawaniwa pia na Leicester City na Arsenal. ***(Calciomercato, via Leicester Mercury)***

### HAVERTZ KUIACHA LEVERKUSEN

KAI Havertz anataka kuondoka Bayern Leverkusen kwa sababu wameshindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo Chelsea inahitaji kuwa na uhakika wa kufuzu ili kumshawishi kiungo huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 21, kumsajili. ***(Bild)***

### WIGAN KUUZA WACHEZAJI

KLABU ya Wigan inaangalia uwezekano wa kuwauza wachezaji wake kadhaa ili kusajili wawili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake. ***(Sun)***

### BAYERN KWA BAKAYOKO

BAYERN Munich inawania kuwasajili viungo wawili kutoka kwenye Ligi Kuu ya England, nyota wa Tottenham, Tanguy Ndombele, 23, na Tiemoue Bakayoko wa Chelsea mwenye miaka 25. ***(Le10Sport)***

### IBRAHIMOVIC BADO KUAMUA

STRAIKA wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, amesema hana uhakika na majaliwa yake kubakia pale AC Milan, kwani hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika hadi sasa kuhusu kuongeza mkataba wake. ***(Sky Sports)***

### MASHABIKI 5,000 RUKSA PSG

MASHABIKI 5,000 waliruhusiwa kuingia uwanjani kushuhudia mchezo wa kwanza wa kirafiki wa kujiandaa na msimu mpya, wakati Paris St-Germain ikiwafunga 9-0 Le Havre. ***(France 24)***

### PELLEGRINI AMUWINDA DIAZ

KOCHA mpya wa Real Betis, Manuel Pellegrini anataka kumsajili kiungo wa Real Madrid, Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 20, kwa mkopo msimu ujao. Pellegrini alifanya kazi na Diaz wakati akiwa Malaga. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### CHELSEA JICHO KWA PELLISTRI

CHELSEA imejiunga na Manchester City na Juventus kwenye mbio za kumwania winga wa Penarol, Facundo Pellistri mwenye umri wa miaka 18 raia wa Uruguay. ***(Calciomercato)***

### GERSON ANOGEWA FLAMENGO

KIUNGO wa Flamengo, Gerson mwenye umri wa miaka 23 raia wa Brazil, ambaye amekuwa akihuishwa na Chelsea na Tottenham, amesema hana mpango wa kuondoka klabuni hapo. ***(Globo Esporte)***

### ZENIT YAMUWANIA LOVREN

ZENIT St Petersburg imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Liverpool na Croatia, Dejan Lovren mwenye umri wa miaka 31. ***(Liverpool Echo)***

HABARI MICHEZO

## Mtemi aipa neno Yanga

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa zamani wa Simba, Mtemi Ramadhani ameitaka Yanga kubadilika kama inataka kwenda sambamba na watani zao Simba, la sivyo watakuwa wakipoteza mechi zao kila wanapokutana nao.

Akizungumzia matokeo ya mechi ya watani wa jadi ya nusu fainali ya Kombe la FA, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Mtemi amesema, Yanga inabidi isajili wachezaji wazuri wenye uwezo mkubwa wa kupambana na wapinzani wao na kimuundo pia.

"Simba imebadilika kimuundo, lakini ina wachezaji wazuri na wenye uwezo mkubwa tofauti na Yanga, hivyo wana kazi kubwa kama wanataka kutawala soka la Tanzania na kuizidi Simba," alisema.

Amesema hata mechi zilizopita za Ligi Kuu ambapo moja zilitoka sare ya mabao 2-2 na nyingine Simba kufungwa bao 1-0, ilitokana na wachezaji wa Yanga kuwa vizuri kimwili kuliko wenzao na si uwezo wa mchezaji mmoja mmoja.

Amesema kuwa kwenye mechi zilizopita ilionekana wachezaji wa Simba hawana stamina na ndiyo maana iliwapa tabu sana kwenye mechi hizo.

## Zimamoto hesabu kwa Malindi leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya Zimamoto, Hassan Abdulrahman, amesema timu zote za Ligi Kuu Zanzibar kwa sasa zinacheza mechi zao kama fainali kutokana na milango ya bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kutokuwa wazi hadi sasa.

Zimamoto ambayo inashika nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo, itashuka dimbani leo Jumanne kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya Malindi iliyopo nafasi ya tisa ikiwa na alama 32.

Akizungumza na gazeti hili juzi, kocha huyo alisema kila timu kwa sasa inacheza kwa ushindani wa hali ya juu katika kipindi hiki cha kuelekea ukingoni na kwamba hakuna ambayo unaweza kuibeza.

Kuhusu mchezo wao wa leo dhidi ya Malindi, kocha huyo alisema utakuwa mgumu kwa sababu wanashuka dimbani wakiwa na malengo ya kusaka ubingwa wakati Malindi wakihitaji kujinusuru na janga la kushuka daraja.

# SAMATTA, COCA-COLA KUIBUA VIPAJI NCHINI

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha vipaji vya soka vinazidi kuibuliwa nchini, Kampuni ya Coca-Cola Tanzania imeingia makubaliano ya kumtumia nahodha wa timu ya Taifa, 'Taifa Stars' na mshambuliaji wa Klabu ya Aston Villa ya Ligi Kuu England, Mbwana Samatta katika kampeni zake ili kuwahamasisha Watanzania kufikia ndoto zao.

**Kwa pamoja, Samatta na Coca-Cola watatumia muungano huo kuwaburudisha na kuwahamasisha Watanzania kufanya kilicho bora ili kuzifikia ndoto zao kimichezo na malengo mbalimbali ya kijamii kwa kupitia kliniki mbalimbali zitakazoandaliwa na kampuni hiyo ya vinywaji baridi.**

"Tangu nilipokuwa mdogo, kila wakati kulikuwa na kitu cha tofauti kuhusu Kampuni ya Coca-Cola. Kwa njia moja, ninahisi ni kama nimeijua Coca-Cola katika maisha yangu yote na ninatambua mashabiki wangu wengi nchini Tanzania na duniani kote wanahisi vivyo hivyo," alisema Mbwana Samatta wakati wa kutangaza ushirikiano huo.

"Ushirikiano huu na Coca-Cola kiukweli ni wa kipekee na wa aina yake, ni zaidi ya kufanya kazi na kampuni inayoongoza kwa utengenezaji wa vinywaji baridi duniani, na ni fursa kuwa sehemu ya kitu kinachougusa ulimwengu."

Aidha, ushirikiano huo umetokana na matarajio na maono ya pamoja ya Samatta na Coca-Cola kutengeneza thamani na kuleta utofauti katika jamii huku ukikusudia kuileta kampuni hiyo ijulikanayo duniani kote 'karibu na nyumbani' kwa kuiunganisha chapa yake ya na nahodha huyo wa Taifa Stars.

Kwa upande wake, Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo, alisema matakwa ya Samatta kuhamasisha, kuunganisha na kuwainua hasa vijana, ni dhihirisho la maadili ya chapa ya Coca-Cola.

"Yeye ni mfano wa kuigwa hapa nchini, anapeperusha bendera ya Tanzania vilivyo ulimwenguni, Ukiangalia historia yake alipotoka kwenye fani hii ya soka na alipofikia, kiukweli inawapa hamasa Watanzania hasa vijana kufuata ndoto zao," alisema Nshimo.

Kampuni ya Coca-Cola imekuwa na historia ndefu ya kuunga mkono michezo, hasa mpira wa miguu katika ngazi zote kuanzia ngazi ya shina, kupitia mashindano yake ya COPA Coca-Cola.

Kwa miaka mingi mashindano haya yametengeneza fursa kwa wachezaji wengi wenye vipaji vya kipekee, kutambuliwa, kuajiriwa na kujiunga na timu ya Taifa ya chini ya miaka 20 ya Tanzania. Mmoja wa wachezaji hao Samatta ambaye alipata bahati ya kushiriki mashindano ya kwanza kabisa ya COPA Coca-Cola nchini Tanzania mwaka 2006 akiwa na timu ya Kimbangulile ya Temeke jijini Dar es Salaam.

"Kama Mtanzania ambaye ni kinara wa Soka katika anga la kimataifa, Samatta anawahimiza vijana wengi kutouchukulia mpira kama mchezo wa kujifurahisha tu, bali kama ajira, na muhimu ni kwamba wanaweza kuzifikia ndoto zao kwa urahisi, kama yeye alivyoweza.

"Kwa kuongezea tu, ni kuwa kupitia kliniki za mpira wa miguu ambazo tutakuwa tunaziandaa, tutaweza kujihusisha na kuwahamasisha vijana wengi zaidi, hii ikiwa sambamba na maono ya Kampuni ya Coca-Cola ya kuburudisha ulimwengu na kuacha alama," alisema Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Kampuni ya Coca-Cola Afrika Mashariki na Kati, Nelly Wainaina.

Alisema Kampuni ya Coca-Cola itaendelea kukuza vipaji vya vijana kupitia ushirika huo na kuamsha matumaini kwa wachezaji chipukizi wa mpira wa miguu kote nchini, huku akiwataka wadau wa michezo nchini kutegemee mengi zaidi kutoka katika muungano huo.




Nahodha wa Taifa Stars na mshambuliaji wa Klabu ya Aston Villa ya Ligi Kuu England, Mbwana Samatta ambaye ameingia makubaliano na Kampuni ya Coca-Cola Tanzania ya kuitangaza chapa ya kampuni hiyo katika kampeni zake ili kuwahamasisha Watanzania kufikia ndoto zao. **PICHA: COCA-COLA**

# Wachezaji Simba kunuka noti, Sven awaonya

**Na Saada Akida**

HUKU ikielezwa kuwa ushindi wa juzi dhidi ya Yanga, umeukuna uongozi wa klabu hiyo na kuahidi 'kuwanukisha' noti wachezaji na benchi la ufundi la timu hiyo, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck amewataka wachezaji wake kutoridhika na kutwaa ubingwa pamoja na kuifunga Yanga na badala yake waelekeza akili na nguvu zao kwenye mechi zao zilizobaki ili kumaliza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa heshima kubwa.

Simba imetinga fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup) kwa kuifunga Yanga mabao 4-1 katika mchezo wa nusu fainali uliochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Sven alisema anawapongeza wachezaji wake kucheza vizuri na kufanikiwa kulipa kisasi kwa kuibuka na ushindi mkubwa katika mchezo huo, lakini akiwataka kutazama zaidi mechi zilizosalia.

Alisema nusu fainali ilikuwa nzuri kwa wapinzani wake kucheza vizuri kipindi cha kwanza pamoja na walivyopata bao la kwanza hali iliyompa wakati mgumu kuhawahimiza wachezaji wake kujitolea.

"Wamejituma wamecheza kwa kiwango kizuri, lakini bado hatujamaliza ligi, tunahitaji kufanya vizuri na kuheshimu ubingwa wetu kwa kutafuta alama muhimu katika mechi zetu za ligi ikiwamo dhidi ya Mbao FC," alisema Sven.

Alisema kwa matokeo hayo pamoja na kutangazwa rasmi mabingwa wa Ligi Kuu, haitawafanya kuridhika, bali wanatafuta pointi zote tatu katika michezo iliyobaki ili kumaliza kwa heshima kubwa.

"Tunakutana na timu iliyopo chini, ipo katika wakati mgumu itakuja kucheza kwa kukamia kumfunga bingwa, lakini pamoja na kutafuta pointi muhimu zitakazowaweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo," alisema kocha huyo.

Wakati Sven akihitaji heshima kwa sasa katika kutafuta pointi 12 katika michezo minne iliyobaki, chanzo chetu ndani ya klabu hiyo kimetueleza kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba chini ya Mwenyekiti wake, Mohamed 'Mo' Dewji, imeahidi kutoa kiasi cha Sh. milioni 400 za Kitanzania kwa wachezaji na benchi la ufundi baada ya kukunwa na kipigo ilichokitoa kwa watani zao, Yanga.


Kikosi cha Simba leo kitaingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao dhidi ya Mbao FC utakaochezwa keshokuwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Michezo
Jumanne Julai 14, 2020
Nipashe



Arteta: Kipigo Spurs majanga Arsenal
UKURASA 22

WAKIMATAIFA...



Winga wa Yanga, Mghana Bernard Morrison, kabla ya mchezo kumkataa na kutolewa uwanjani, akipambana na kiungo mshambuliaji wa Simba raia wa Msumbiji, Luis Miqussone kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi. Simba ilishinda 4-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Morrison ajikaanga, mguu ndani, nje

**Na Shufaa Lyimo**

KITENDO cha mchezaji wa kimataifa wa Yanga, winga Mghana Bernard Morrison, kufanyiwa mabadiliko katika mechi dhidi ya Simba juzi na kuamua kutoka moja kwa moja uwanjani badala ya kukaa kwenye benchi na wenzake, kimeukera uongozi wa Yanga na kuahidi kujifungia kumjadili kabla ya kutoa uamuzi mzito dhidi yake.

Katika mechi hiyo ya nusu fainali ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi na Simba kushinda 4-1, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael alimtoa Morrison dakika ya 79 na nafasi yake kuchukuliwa na Patrick Sibomana, lakini winga huyo hakukaa katika benchi na kuamua kutoka moja kwa moja uwanjani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mshindo Msolla alisema mchezaji huyo ameonyesha utovu mkubwa wa nidhamu, kitendo ambacho hakijawapendeza wadau wa soka na kuahidi kulitolea maamuzi haraka iwezekanavyo.

"Morrison ameonyesha utovu wa nidhamu kwa kitendo cha kutolewa na kocha na kuamua kutoka nje ya uwanja badala ya kukaa na wachezaji wenzake kwenye benchi, tutakaa sisi kama viongozi tutajua nini tunatakiwa kukifanya," alisema Msolla.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Boniface Mkwasa alisema hajafurahishwa na kitendo alichokifanya mchezaji huyo na kuwataka wachezaji wengine kuwa makini pindi wanapokuwa uwanjani ili kujiepusha na masuala kama hayo ambayo hayana afya kwao.

# Yanga: Sababu kipigo Simba hii

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

## Eymael asema subirini msimu ujao, ageukia pointi 12 huku wachezaji na uongozi wakiomba radhi...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amesema alijua mchezo wao dhidi ya Simba kwenye Kombe la FA juzi utakuwa mgumu, lakini hakutarajia timu yake kuchapwa 4-1, huku akieleza moja ya sababu iliyochangia kipigo hicho ni kutokana na baadhi ya wachezaji wake kutokuwa fiti kwa asilimia mia.

**Akizungumza na gazeti hili, Eymael alisema nyota wake, Nahodha Papy Kabamba Tshishimbi na Haruna Niyomzima hawakuwa kwenye ubora wao kwa kuwa wametoka kwenye chumba cha majeruhi.**

"Lakini baadhi ya wachezaji wangu hawakufuata maelekezo yangu, nilitegemea mchezo mgumu, lakini mabao tuliyofungwa yalikuwa mengi na hatukucheza kwenye ubora wetu," alisema Eymael.

Aidha, alisema kuwa Simba walikuwa bora zaidi eneo la katikati na hata safu yao ya ushambuliaji ilikuwa kwenye ubora na kuwapa kazi kubwa mabeki wake.

"Makosa yanatokeo kwenye mpira na unapokutana na timu bora inakuadhibu kutokana na makosa yako, kwa sasa tutapambana kuhakikisha tunamaliza vizuri michezo iliyobaki ya Ligi Kuu," alisema Eymael huku akiahidi kutengeneza timu ya ushindani msimu ujao.

Eymael alisema hakufurahishwa na kiwango cha wachezaji wake walichocheza katika mchezo huo, lakini akiwataka sasa kuweka nguvu katika michezo iliyobaki ya ligi ili kushika nafasi ya pili ambayo kwa sasa inashikiliwa na Azam FC. Alisema baada ya kukosa nafasi ya kuiwakilisha nchi katika michuano ya kimataifa wanafanyia kazi mapungufu yao kwa ajili ya kuwania nafasi ya pili ambayo itakuwa ya heshima kwao.

"Simba walituzidi na kutumia makosa yetu kutufunga, pia sijafurahishwa na matokeo pamoja na jinsi wachezaji wangu walivyocheza kwa kiwango cha chini, sasa nimewataka kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo minne iliyobaki," alisema Eymael.

Kwa upande wa beki wa timu hiyo, Lamine Moro amekiri timu yao kuzidiwa katika mchezo huo dhidi ya Simba kwa kutumia makosa yao kupata ushindi mkubwa.

"Tumepokea matokeo, mchezo wa soka una matokeo ya kufungwa, kushinda na hata sare, wenzetu walitumia mapungufu yetu, sasa tunaendelea na mapambano katika michezo iliyobaki kutafuta alama muhimu ili tumalize ligi katika nafasi ya pili," alisema beki huyo.

Katika hatua nyingine wachezaji na uongozi wa klabu ya Yanga umewaomba radhi wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kutokana na kipigo hicho cha juzi.

Naodha msaidizi wa klabu hiyo, Juma Abdul, alisema matokeo waliyoyapata yamewaumiza sana na yametokana na makosa yao wachezaji uwanjani.

"Kwa niaba ya wachezaji wenzangu, nawaomba radhi wanachama na mashabiki wa klabu yetu kutokana na matokeo haya, ni kweli yanaumiza na hatukupaswa kuyapata," alisema Abdul.

Wakati Abdul akisema hivyo, Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Simon Patrick, aliungana na nahodha huyo kuwaomba radhi mashabiki na kuwataka kuendelea kushikamana mpaka msimu utakapomalizika.

"Tumeona mapungufu ya kikosi chetu, tuendelee kushikamana kama klabu na haya yote yatafanyiwa kazi mwishoni mwa msimu huu ili msimu ujao tuwe na kikosi imara kitakachotupa furaha, uongozi unawaomba radhi mashabiki na wanachama wetu kwa matokeo haya," alisema.

Yanga imebakiza michezo minne ambapo kesho itaikaribisha Singida United ambayo tayari imeshashuka daraja, Julai 18 itaialika Mwadui FC, kabla ya kuifuata Mtibwa Sugar na kisha kufunga msimu ugenini dhidi ya Lipuli FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >